**Jumatano Januari 29, 2025** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581936 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US Nipashe digital

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

UKURASA WA 3

**Lissu**, Heche kutinga rasmi makao makuu CHADEMA leo

UKURASA WA 18

**Kampeni** msaada kisheria ya Samia yatua Kilimanjaro, wakazi kunufaika

UKURASA WA 19

**Uamuzi** wa Trump USA kujitoa WHO kuathiri miradi ya usalama barabarani



**VAN DIJK: BADO SIJUI HATIMA YANGU LIVERPOOL**

UKURASA 22

## MKUTANO WA NISHATI

# Marais Afrika waridhia Azimio la Dar kimkakati

• **WB**, OPEC, AfDB waanza kumwaga fedha kusaidia miradi ya 'Mission 300'... *Uk. 2 & 4*



Rais Samia Suluhu Hassan (katikati), akiwaongoza viongozi mbalimbali kuonyesha mkataba wa Azimio la Dar es Salaam, wakati wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watanzania waliokwama vitani DRC waokolewa

**Na Maulid Mmbaga**

VITA vimeendelea kushuhudiwa katika mji wa Goma Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) huku zaidi ya Watanzania 43 waliokwama na kuomba msaada kutokana na kuzingirwa na milio ya risasi wakifanikiwa kukimbilia Rwanda.

Machafuko katika mji huo yameendelea baada ya waasi wa M23 ambao inadaiwa kuwa wanashirikiana na wanajeshi wa Rwanda kuiteka Goma juzi na kuwalazimisha wanajeshi wa Kongo kujisalimisha, hali ambayo imesababisha wakazi kulikimbia eneo hilo.

Ilielezwa kuwa awali Watanzania hao walikuwa katika eneo la Jambo Safari karibu na Uwanja wa Ndege wa Goma walilazimika kuomba msaada wakihofia kuuliwa na waasi wa M23 baada ya kuvamia eneo hilo.

ENDELEA UKURASA 19

# Wastaafu Jeshi la Polisi wadai bilioni 97.12/-

UKURASA 7

**MICHEZO** **STARS: HATUIHOFII NIGERIA, TUNISIA AFCON** UK.24

**MAONI,** UK.6




Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga (kulia) na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina, wakibadilishana mikataba, baada ya kutiliana saini makubaliano ya Azimio la Dar es Salaam, wakati wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

MKUTANO WA NISHATI

# Marais Afrika waridhia Azimio la Dar kimkakati

**Na Elizabeth Zaya**

WAKUU wa Nchi na Serikali za Afrika wameridhia Azimio la Dar es Salaam linalolenga kuwahakikishia upatikanaji umeme watu milioni 300 barani Afrika kufikia mwaka 2030.

Viongozi hao wametaja hatua hiyo ni muhimu katika kushughulikia changamoto kubwa za nishati ambazo zinakwamisha maendeleo ya Afrika.

Yaliyomo katika azimio hilo ni pamoja kila nchi kushiriki kugharamia upatikanaji nishati ya umeme na kujenga uwezo ili kuhakikisha utekelezaji miradi ya upatikanaji umeme kwa wakati.

Azimio linasisitiza usawa wa kijinsia katika kuongeza upatikanaji nishati, hasa kwa wanawake na wafanyakazi ili kusaidia kukuza mustakabali wa nishati endelevu.

Tamko la azimio hilo linaainisha umuhimu wa kuunganisha nishati hiyo kwenye kanda za nchi hizo, kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kama vile jua, upepo, umeme wa maji, joto la ardhi na nishati yote mchanganyiko ili kuwa na nishati imara.

Azimio hilo linatoa wito wa ushiriki mkubwa wa sekta binafsi kupitia na kuongeza ubunifu na kuweka mazingira bora ya kisheria ili kusaidia kufungua maendeleo, kuboresha miundombinu na kuleta mageuzi ya nishati kote barani Afrika.

Viongozi hao pia wamekubaliana kuundwe Tume ya Umoja wa Afrika ambayo itasaidia kuratibu na kufuatilia utekelezaji azimio hilo, shabaha ikiwa kumaliza kabisa tatizo la umeme katika nchi zao na kuimarisha uchumi wa nchi hizo.

Wamekubaliana pia kuhakikisha upatikanaji umeme na nishati safi ya kupikia, kutumia nishati mbadala na nishati mchanganyiko huku wakiongeza uhamasishaji na kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Wakuu hao wamekubaliana kuongeza ufanisi, kupanua na kuboresha miundombinu ya uzalishaji umeme, upitishaji na usambazaji nishati kwa gharama shindani na gharama nafuu katika kanda hizo.

Viongozi hao pia wamekubaliana kuweka mipango, kanuni na mifumo ya nishati inayozingatia michakato ya ununuzi shindani na wazi, kuratibu mipango ya upitishaji, viwango vya bei na kanuni za gridi pamoja na kukuza ushirikiano kati ya nchi hizo.

Vilevile, wamekubaliana kuvutia mitaji kutoka sekta bianfsi na kuhakikisha fedha zinapatikana kwa ajili ya kuleta mabadiliko kwenye mifuko ya nishati, kupokeza ahadi za wadau wa maendeleo.

Azimio hilo linalenga kutekeleza mpango wa AIDA na IDF na mpango wa maendeleo wa kuwa na malengo ya muda mrefu na upatikanaji fedha kwa ajili ya miradi ya muda mrefu kuhakikisha nishati safi inapatikana.

"Wakati lengo letu likiwa ni kufikia watu milioni 300, tunapendekeza hatua madhubuti na ushirikiano wa kisiasa katika kutekeleza. Tunaomba Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuwezesha utekelezaji azimio hili kwa ajili ya kupeleka kwenye mkutano wa AU kwa ajili ya kujadili na kupitisha," inasomeka sehemu ya azimio hilo.

Mkutano wa Nishati wa Mission 300, umefanyika nchini kwa siku mbili kuanzia juzi, ukihudhuriwa na wakuu wa nchi 24 za barani Afrika pamoja na mawaziri wa nishati na fedha pamoja na viongozi wakuu wa taasisi za fedha za kimataifa. Jumla ya viongozi 2,600 wameshiriki mkutano huo.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# ...Wadau maendeleo waanza kumwaga fedha 'mission 300'

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa maendeleo, wameanza 'kumwaga' fedha zitakazosaidia kutekeleza mpango wa 'mission 300' wa kufikisha umeme kwa watu milioni 300 katika bara la Afrika.

Walitoa ahadi ya kuanza kutoa fedha hizo wakati wakizungumza mbele ya marais walioshiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati, uliomalizika jana, jijini Dar es Salaam.

Wadau hao ni Benki ya Maendeleo ya Afrika(AFDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Kiislam, Shirika la Maendeleo ya Miundobinu na Mfumo wa Kimataifa unounganisha nchi zinazouza mafuta (OPEC).

Rais wa AFDB, Dk. Akinwumi Adesina na WB, alisema wametenga Dola za Marekani bilioni 40 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mpango wa awali wa mpango huo wa Mission 300 wa kufikisha nishati ya umeme kwa wananchi milioni 300 katika nchi za Afrika.

Kati ya hizo, Dola bilioni 22 zitatolewa na WB na Dola bilioni 18.2 zitatolewa na AFDB.

Kadhalika, alisema Rais wa Benki ya Kiislamu ameahidi kutoa Dola bilioni 2.6, Rais wa Maendeleo ya Miundombinu akiahidi kutoa Dola bilioni 1.5 na Rais wa Mfuko wa OPEC akiahidi kutoa Dola bilioni moja.

Dk. Adesina, alisema upatikanaji wa umeme ni nyenzo muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ukosefu wa nishati hiyo unapunguza ukuaji wa uchumi kwa asilimia 2.4.

Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Amina Mohamed, aliipongeza Tanzania kwa kupanua huduma ya upatikanaji wa nishati ya umeme, ikiwamo kuwekeza katika nishati mbadala na kwamba sio tu kutakuza ukuaji wa uchumi, lakini pia kutachochea upatikanaji wa ajira.

Alisema katika kipindi cha zaidi ya muongo mmoja, Tanzania imeongeza kasi ya upatikanaji wa umeme, kutoka asilimia 14 mwaka 2011 hadi 46 mwaka 2022.

Alisema nchini Tanzania, zaidi ya taasisi za kijamii 60,000 zikiwamo shule 12,905, vituo vya kutolea huduma za afya 6,768 na sehemu za kazi zaidi ya 8,000 zimeunganishwa na umeme wa uhakika.

Alisema mikakati ya nchi hiyo kuhamasisha nishati mbadala ni miongoni mwa kichocheo cha mabadiliko ya kiuchumi barani Afrika.

**MIPANGO YA TANZANIA**

Rais Samia Suluhu Hassan alisema Tanzania ni moja ya nchi 12 zinazotekeleza mpango mahsusi wa taifa kuhusu nishati ambao utaongeza kasi katika kuunganisha umeme nchini hadi kufikia asilimia 72 ifikapo mwaka 2030.

Alisema ili kufanikisha mpango huo ndani ya miaka mitano, inahitaji uwekezaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni tano zitakazopatikana kutoka katika sekta binafsi.

Pia, alisema kupitia mpango huo, Tanzania imejipanga kutekeleza mambo manne ikiwamo kuongeza uzalishaji wa umeme kutokana na nishati mchanganyiko kwamba mpaka sasa ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,431 na asilimia 58 inatokana na vyanzo vya maji, 35 gesi asilia na saba kutoka vyanzo vingine.

Kadhalika, Tanzania imelenga kuongeza megawati 2,463 za nishati kutokana na jua, gesi asilia, upepo na vyanzo vingine ifikapo mwaka 2030.

Alisema mweleko wa Tanzania kwa sasa ni kufikisha vitongoji 64,359 na mpaka sasa imeshavifikia vitongoji 32,827.

Aidha, Tanzania ni kiungo muhimu katika kuunganisha nishati kwa nchi nyingine za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (SADC) na kuwezesha biashara ya umeme kutoka Afrika Kusini hadi Cairo nchini Misri.

Tayari Tanzania imeunganisha miundombinu ya umeme katika nchi za Burundi, Rwanda na Kenya na sasa inaendelea kuunganisha katika nchi ya Zambia na Uganda na kwamba uwapo wa miundombinu hiyo utawezesha biashara ya nishati katika nchi za Jumuiya ya Afrika na SADC.

Rais Samia alisema nchi yake imeweka mkakati wa taifa wa nishati safi kupikia unaolenga kupandisha kiwango cha matumizi ya nishati hiyo safi ya kupikia kutoka asilimia 10 hadi asilimia 80 ifikapo mwaka 2030 na mpango mahsusi uliozinduliwa jana utasaidia kufikia lengo hilo.

## HABARI KITAIFA

# Mbunge ahoji mpango serikali kukabili wizi na utekaji watu

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu, amehoji serikali imejipangaje katika kudhibiti matukio ya wizi wa watu au utekaji nchini.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge huyo alisema mkoa wa Iringa ni moja ya waathirika na matuko hayo na wamepoteza vijana wawili, Banis Nyato na Ali kwa kutekwa.



Kutokana na swali hilo, Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson alimtaka Mbunge kuwasilisha swali hilo kama swali la msingi ili serikaitoe majibu kikamilifu.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Rorya (CCM), Jafari Chege, alihoji lini wizi wa mifugo utadhibitiwa wilayani Rorya.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, alisema Jeshi la Polisi lina wajibu wa kudhibiti wizi wa mifugo katika wilaya ya Rorya.

Alisema jitihada zinazofanywa na Jeshi la Polisi ni pamoja na kutoa elimu juu ya ulinzi jirani, kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi na mazizi salama.

"Juhudi zingine ni kuimarisha kikosi cha kupambana na wizi wa mifugo (STPU ) kwa kuongeza askari na vitendea kazi, kufanya mikutano ya ujirani mwema na polisi wilaya ya Nyatike ya nchini Kenya juu ya udhibiti wa makosa yanayovuka mipaka na jitihada zote hizi ni endelevu na zimepunguza kwa kiasi kikubwa wizi wa mifugo," alisema.

Hata hivyo, alisema takwimu zinaonyesha katika kipindi cha Desemba, 2023 na mwezi Januari, 2024 kumeripotiwa matukio 26.

Pia alisema kwa kipindi kama hicho Desemba, 2024 na Januari, mwaka huu, matukio hayo yamepungua na yaliyoripotiwa ni tisa ikilinganishwa na mwaka uliopita.

# Lissu kutinga rasmi makao makuu ya CHADEMA leo



**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI mpya wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, atapokewa rasmi leo katika makao makuu ya chama hicho, Mikocheni mkoani Dar es Salaam.

Kiongozi huyo ataambatana na Makamu Mwenyekiti, John Heche na Naibu Katibu Mkuu Bara, Amani Golugwa na atapokewa na Katibu Mkuu, John Mnyika, na watendaji wa makao makuu ya chama hicho saa 5:00 asubuhi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana na Msaidizi wa Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, Apolinary Margwe, chama kinawakaribisha viongozi wakuu wa chama kutoka Zanzibar, viongozi wakuu wa mabaraza ya chama, Kanda ya Pwani na maeneo mengine kujitokeza kumsindikiza mwenyekiti.

Lissu alichaguliwa na mkutano mkuu wa CHADEMA uliofanyika Januari 21, mwaka huu, Dar es Salaam ikiwa ni miaka 32 tangu kuanzishwa kwa chama hicho.

Katika uchaguzi huo, Lissu aliibuka mshindi kwa kupata kura 513 na aliyekuwa anayetetea nafasi yake, Freeman Mbowe ambaye ameongoza kwa miaka 21 alipata kura 483 huku mgombea mwingine Odero Charles akipata kura moja.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 4(1&2(b)) ya Kanuni za Mafuta (Gesi Asilia) (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji) ya Mwaka 2018**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya **Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited** kwa ajili ya kibali cha ujenzi wa bomba la gesi asilia lenye urefu wa mita 20. Bomba hilo litajengwa kutoka barabara ya NIDA Textile hadi kituo kipya cha gesi asilia cha Rafiki One kilichopo eneo la Tabata (NIDA Textile), kandokando ya barabara ya Mandela, Mkoa wa Dar Es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**

**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

183451



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari kutoka kampuni ya NatEnergy Tanzania Company Limited kitakacho jengwa kandokando ya barabara ya Kibada katika kiwanja Namba 4 Kitalu F, Mtaa wa Uvumba, kata ya Kibada, Manispaa ya Kigamboni, Dar es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**

**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

183451

HABARI PICHA

# MKUTANO WA NISHATI WA WAKUU WA NCHI ZA AFRIKA JIJINI DAR ES SALAAM




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Nchi ya Madagascar, Andry Rajoelina katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**




Naibu Waziri Mkuu na Waziri Nishati, Dk. Doto Biteko, akizungumza wakati wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, akizungumza na Naibu wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Amina Mohamed, katika mkutano huo. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Benki ya Dunia, Ajay Banga pamoja Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinumwi Adesina, kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika, jana. **PICHA: IKULU**



Wakuu wa nchi kutoka mataifa mbalimbali na washiriki wengine wakifuatilia mkutano huo, jana. **PICHA: IKULU**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia), akizungumza na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bo Li, kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika jana. **PICHA: OMR**

## TANGAZO

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFAZA FEDHA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### BANK OF INDIA (TANZANIA) LIMITED
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2024
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-24 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-24 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,986 | 2,613 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,703 | 11,587 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 49,664 | 49,084 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,680 | 2,298 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 5,790 | 4,077 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 104,261 | 119,280 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,590 | 4,447 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,412 | 1,454 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **178,086** | **194,842** |
| **B.** | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 2,681 | 28,087 |
| 18 | Amana za Wateja | 127,439 | 119,698 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 170 | 328 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 26 | 28 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,725 | 3,895 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 302 | 560 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **134,342** | **152,596** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **43,744** | **42,246** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 5,014 | 5,014 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 13,777 | 13,777 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,454 | 1,956 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **43,744** | **42,246** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 24,273 | 20,904 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,792 | 6,982 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,102 | 2,596 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 24.56% | 21.68% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.50% | 5.73% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 81.74% | 82.47% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 58.55% | 61.22% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 90.86% | 89.84% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -11.95% | 1.41% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -8.60% | 1.52% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2024
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2024** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.10.2024** | **21,500** | - | **15,732** | **5,014** | - | - | **42,246** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,499 | - | - | - | **1,499** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | - | - | | | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.12.2024** | **21,500** | - | **17,231** | **5,014** | - | - | **43,744** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2024** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.07.2024** | **21,500** | - | **16,564** | **3,753** | - | - | **41,817** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 429 | - | - | - | **429** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,260) | 1,260 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.09.2024** | **21,500** | - | **15,732** | **5,014** | - | - | **42,246** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2024
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka wa sasa 31-Dec-24 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 4,410 | 4,444 | 17,973 | 16,300 |
| 2 | Gharama za Riba | 2,043 | 2,294 | 8,563 | 8,091 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba ( 1kutoa 2)** | **2,366** | **2,150** | **9,409** | **8,209** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | (97) | (1,424) | (285) | (2,265) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 189 | 814 | 1,271 | 2,713 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba :** | **861** | **636** | **1,872** | **1,657** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 361 | 109 | 699 | 343 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 500 | 527 | 1,173 | 1,314 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,771** | **1,728** | **6,653** | **6,086** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 739 | 809 | 3,303 | 2,978 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 1,032 | 919 | 3,350 | 3,108 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,364** | **1,668** | **3,642** | **3,332** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (135) | 38 | 188 | 441 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,499** | **1,630** | **3,454** | **2,890** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka** | **1,499** | **1,630** | **3,454** | **2,890** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 34 | 34 | 34 | 34 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 279 | 303 | 161 | 134 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.93% | 3.52% | 1.91% | 1.77% |
| (ii) | Wanahisa | 13.94% | 16.20% | 8.22% | 7.38% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 33.60% | 34.02% | 33.53% | 33.89% |
| (iv) | Zinazozalisha | 5.65% | 5.01% | 5.44% | 5.00% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2024
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-24 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-24 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,364 | 564 | 3,642 | 3,332 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 322 | 672 | 1,961 | 173 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 14,876 | (1,532) | 4,870 | (10,308) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | (1) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (17,666) | 2,055 | (15,524) | 9,265 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (13,140) | 6,145 | 418 | (921) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (588) | 428 | (725) | 408 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (145) | (776) | 2,961 | (1,626) |
| | - Kodi Iliyolipwa | 135 | (135) | (188) | (1,391) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(14,843)*** | ***7,421*** | ***(2,585)*** | ***(1,068)*** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (145) | - | (164) | (229) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | (28) |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(145)*** | - | ***(164)*** | ***(257)*** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | (989) | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - | ***(989)*** | - |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(14,987)** | **7,421** | **(3,738)** | **(1,324)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 33,854 | 26,433 | 22,604 | 23,928 |
| | **Mwaka** | **18,866** | **33,854** | **18,866** | **22,604** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2024

**Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Mr. Ashish Kumar Jha**<br>**Mkurugenzi Mkuu** | | **28.01.2025** |
| **Mr. Mahadhil M.Karwani**<br>**Mkuu wa Fedha** | | **28.01.2025** |
| **Mr. Allen Richard**<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | **28.01.2025** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **1. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi** | | **28.01.2025** |
| **2. Dr. Paul Kato - Mkurugenzi** | | **28.01.2025** |

183456

## MAONI & UCHAMBUZI

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Ufadhili usambazaji nishati safi kupikia upewe msisitizo*

**SUALA** la upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ni ajenda kubwa duniani kote likiwa na lengo la kuhakikisha watu wengi wanatumia aina hiyo ya nishati kwa manufaa ya kiafya, kiuchumi na kupunguza kasi ya matumizi ya mkaa na kuni kwa ajili ya kupikia pamoja na uharibifu wa mazingira.

Tangu alipoingia madarakani takriban miaka minne iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan ameweka kipaumbele suala hilo na amekuwa kinara katika kuhimiza matumiai ya nishati safi kwa Afrika nzima. Hatua ya Rais Samia kuipa kipaumbele ajenda hiyo ni kutokana na madhara ya kiafya na kiuchumi kwa wanadamu hasa wanawake.

Kwa mazingira ya kawaida na maisha ya kiafrika, mwanamke ndani ya nyumba ndiye mwenye wajibu mkubwa wa kuhakikisha huduma za familia kama vile chakula, maji na nishati kupikia zinapatikana. Kwa mantiki hiyo, mwanamke hutumia muda mwingi kwa ajili ya kutafuta kuni au mkaa kwa ajili ya kupikia chakula cha familia na matokeo yake, anashindwa kufanya kazi za uzalishaji ili kujikwamua kiuchumi binafsi, familia na jamii kwa ujumla.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, serikali imeweka kipaumbele kuhusu upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ili kuokoa muda wa kutafuta nishati ya kupikia hasa kuni na mkaa ambayo si salama kwa afya ya mtumiaji na pia inachangia kasi ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Serikali, katika kutimiza ajenda hiyo ambayo inapewa kipaumbele na Rais mwenyewe, imeandaa mkakati wa miaka 10 ya nishati safi ya kupikia kuanzia mwaka 2024 hadi 2024. Kwa mujibu wa takwimu matumizi ya nishati safi ya kupikia yameongeza kwa kasi ndogo kutoka asilimia 1.5 mwaka 2010 hadi asilimia 6.9 mwaka 2021. Takwimu hizo ziko chini sana ya matumizi ya kidunia ya wastani wa asilimia 71 katika kipindi hicho.

Hali hiyo inaonesha jitihada kubwa zinatakiwa kufanyika ndiyo maana serikali katika mkakati huo, imedhamiria kuwa asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati hiyo ifikapo wakati huo. Mkakati huo pia unaendana na lengo Namba 7 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ya Umoja wa Mataifa la kuhakikisha upatikanaji wa nishati nafuu, inayopatikana kwa urahisi, endelevu na ya kisasa kwa wote.

Tangu kuanza kwa utekelezaji wa mkakati huo, serikali imeweka juhudi kubwa katika kuhakikisha Watanzania wengi wananufaika na matumizi ya nishati safi ya kupikia na kampuni kadhaa zinazouza nishati hiyo hasa gesi ya kupikia zimepewa nafasi ya kusambaza. Pamoja na kupewa nafasi hiyo, tatizo kubwa limekuwa uwezo wa kifedha katika kufikia azma ya kuwapatia wahitaji aina hiyo ya nishati, hivyo kuhitaji mikopo kutoka taasisi za fedha.

Hatimaye kilio hicho kimewafikia wadau hasa taasisi za fedha kuanza kutoa mikopo kwa ajili ya usambazaji wa nishati safi. Benki ya NMB imekuwa mfano kwa kutoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya kukopesha wasambazaji wa gesi ya kupikia kwa lengo la kufanikisha azma hiyo ya serikali.


Ni dhahiri kwamba kiasi hicho cha fedha kitachochea kasi ya usambazaji wa gesi ya kupikia kwa Watanzania wengi kupitia kampuni zilizopewa kazi hiyo kupitia mikopo yenye riba nafuu ya benki hiyo. Kwa mantiki hiyo, kutakuwa na kasi zaidi ya kupatikana kwa gesi hiyo hadi maeneo ya vijijini ambako ndiko kwenye tatizo kubwa la utumiaji wa nishati isiyo safi hasa kuni na mkaa ambayo ni hatarishi kwa afya na maisha ya watumiaji.

Pamoja na ukweli huo, ni vyema serikali ikatoa garantii kwa kampuni zinazosambaza gesi ya kupikia pamoja na zile zinazotengeneza majiko banifu na sanifu ili zipate mkopo nafuu kupitia taasisi za fedha, hasa benki kama ilivyofanyika kwa NMB.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# *Hongera serikali umeme nchi nzima*

**UMEME** ni muhimu kwa maendeleo ya nchi kuanzia uchumi kwenye viwanda, biashara na kilimo mashambani.

Ni nguzo upatikanaji na utoaji huduma zote kuanzia mawasiliano, elimu, afya, usafirishaji na maji katika maeneo yote mijini na vijijini ambako shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na kutoa huduma zinafanyika.

Tanzania imevisambazia umeme vijiji vyote 12,318 na vitongoji kadhaa. Aidha, inatazamia kuongeza uwezo wa taifa wa kuzalisha umeme zaidi ufikie megawati 4,000 ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere kwenye Mto Rufiji linatarajiwa kuzalisha megawati 2,100 na mwaka jana ilishuhudiwa mitambo yenye uwezo wa kuzalisha megawati 1,400 ikifanya kazi.

Katika mkutano wa siku mbili wa 'Nishati Afrika' uliomalizika jijini Dar es Salaam jana, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, anataja mafanikio mengi yaliyopatikana kitaifa.

Ni kusanyiko linawakutanisha marais kutoka nchi 24, mawaziri na wadau wa taasisi za fedha za kimataifa.

Anayesema hayo katika mkutano huo na kutaja maendeleo yaliyofikiwa na mataifa ya Afrika tangu mwaka 1960.

Katika ufafanuzi wake anasema Tanzania imeongeza uzalishaji wa nishati hiyo kutoka megawati 21 wakati wa uhuru hadi 3,160 na sasa imepiga hatua zaidi hadi kila kijiji kuwa na umeme.

Hiyo ni hatua ya kupongeza ambayo nchi imefikia ila ombi langu ni kwamba kasi ya kuimarisha upatikanaji wa nishati hiyo iongezeke, kwani kumekuwapo na tatizo la katizo la umeme kila mara.

Tanzania ina vyanzo mbalimbali vya nishati, vingezidi kuimarishwa ili kuwa na umeme wa uhakika ambao hauna changamoto utakaoweza kuuzwa nchi jirani na kuliongezea taifa mapato.

Kwa sasa Tanzania inaimarisha muunganiko wa Afrika au gridi ya Afrika, kwa miundombinu ya umeme inayounganisha Kenya, Burundi, Rwanda na Uganda, ikiwa mbioni kuiunganisha na Zambia.

Hayo yakifanyika, nchi itakuwa na umeme wa kutosha, kwani hata Naibu Waziri Mkuu anakiri kwamba pamoja na maendeleo ya nishati taifa linayo ya kujivunia, bado inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati.

Ni wazi matarajio ya kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda, madini na huduma nyingine ni jambo ambalo linahitaji uwekezaji wa kimkakati zaidi katika sekta ya nishati kama anavyosema.

Umeme unahitajika kila mahali kuanzia hospitalini, uzalishaji viwandani, miundombinu ya usafiri na mawasiliano, darasani kufundisha wanafunzi, mashambani kwenye kilimo na jikoni kuandaa vyakula.

Ni hatua muhimu kwa nchi za Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara kuweka mikakati ya kuhakikisha watu wake wanapata nishati hiyo.

Katika mkutano huo uliomalizika jana, imeelezwa kuwa wananchi

wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa nishati hiyo na takribani Waafrika milioni 600 haujawafikia.

Wapo wengine wamegeukia nishati mbadala ikiwamo ya mionzi ya jua au sola kwa ajili ya matumizi ya kila siku.

Afrika inatamani ifikapo mwaka 2030, watu milioni 300 wawe na nishati hiyo, huku njia mojawapo inayotajwa ya kufanikisha hilo ni kuunganisha nguvu na kushirikiana kupitia sekta ya nishati ili bara lifikie lengo hilo na kubadili sura yake.

Inaelezwa kuwa maendeleo yaliyofikiwa na mataifa ya Afrika tangu mwaka 1960, ni pamoja na Tanzania kuongeza uzalishaji wa nishati hiyo kutoka megawati 21 wakati wa uhuru hadi megawati 3,160.

Kimsingi, hiyo ni hatua ya kujipongeza hasa baada ya kufikisha umeme kila kijiji ili wakazi wa huko waweze kutumia umeme kujiletea maendeleo badala ya kuendelea kubaki nyuma.

Wanaoishi vijijini, wanaweza kutumia nishati hiyo kwa kuanzisha viwanda vidogo hata vya kusindika matunda, kuwa na mashine ya za kusaga nafaka, saluni za wanawake kwa wanaume, kuchomelea vyuma na migahawa ya vyakula na vinywaji kwa kutumia jokofu.

# Wastaafu polisi wadai bilioni 97/-

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi imesema askari polisi wastaafu wanadai kiasi cha Sh. bilioni 97.12 na kwamba serikali inaendelea na hatua mbalimbali za kulipa madai hayo.

Naibu Waziri Daniel Sillo aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Maida Hamad Abdallah. Mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itawalipa madai ya muda mrefu askari polisi waliomaliza muda wao wa utumishi.

Akijibu swali hilo, Sillo alisema serikali inaendelea kulipa madai ya askari polisi waliomaliza muda wao wa kazi baada ya kustaafu wanadai Sh. 97,120,011,700.26.

Alisema mpaka sasa madai yaliyohakikiwa na kuwasilishwa Wizara ya



Fedha kwa ajili ya malipo ni Sh. 75,214,744,005.10.

"Kwa sasa madai yanayoendelea kuhakikiwa ni ya mwaka wa fedha 2023/24 na Sh. 21,905,267,695.16 zinadaiwa. Pindi uhakiki ukikamilika, madai yote yatawasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asha Abdallah Juma, alihoji kwa nini mifumo ya kielektroniki isitumike kuweka taarifa zote muhimu za askari ili atakapofika umri wa kustaafu, asisotee malipo.

"Kumekuwa na mlolongo mkitaka athibitishe aliajiriwa lini, alipandishwa cheo lini na alikopa kitu gani huu ni usumbufu. Pia serikali inatambua kuwa askari hao kwa sasa wanahitaji hayo mafao kushinda siku nyingine yoyote," alisema.

Akijibu swali hilo, Sillo alisema serikali imeendelea kufanya kazi kubwa ya mifumo ya kielektroniki kuhakikisha taarifa zote za askari zinaingia kwenye mfumo, ili kuepusha usumbufu wanapomaliza muda wao wa utumishi ili walipwe kwa wakati.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Wakili asema ubambikaji kesi unawaumiza wananchi wengi

**Na Grace Gurisha**

WAKILI wa Kujitegemea, Dk. Aloys Rugazia, amesema jinai za kuoneana na kubambikiana kesi ni eneo linalosumbua watu wengi katika jamii na wananchi wengi wanalalamika kuhusu jambo hilo.

Ametaja changamoto zingine ambazo wananchi wanapata ni migogoro ya ardhi na mirathi, wajane, wazee na watoto yatima wanapata shida kupata haki zao za msingi kwa wakati.

Dk. Rugazia alisema hayo juzi kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Kibasila, Dar es Salaam wakati wa maandalizi ya kutoa elimu ya sheria bila malipo na kuandaa nyaraka katika kuadhimisha Wiki ya Sheria kwa lengo la kuwafikia wananchi ambao hawana fedha za kupata huduma za sheria.

"Ardhi ni maisha, ni moja kati ya mali muhimu katika mustakabali wa watu. Mara nyingi ardhi imekuwa inaleta msuguano kati ya walio nacho na wasio nacho. Mara nyingi wanajikuta katika hali ngumu ndiyo maana kwa wiki hii tunatoa msaada bure, watu waje.

"Eneo la jinai za kuoneana na kubambikiana kesi linasumbua watu wengi katika jamii. Hii tumekutana nayo pale wananchi wanapokuwa wanatafuta msaada wa kisheria ndipo wanatueleza hayo," alisema Dk. Rugazia.

Alisema wako kwenye Wiki ya Sheria ambayo ilizinduliwa Januari 25, mwaka huu. Wanaifikia jamii kuhakikisha inapata haki kwa sababu siyo kila mtu ana uwezo wa kulipia gharama za kupata huduma za kisheria.

"Hivi karibuni Rais alianzisha Mama Samia Legal Aid, mpango mkakati wa kutoa msaada wa kisheria kwa watu ambao tunaishi nao katika jamii yetu na kwa namna moja au nyingine wana kiu ya haki, lakini hawawezi kuipata.

"Mimi nikiwa kama Managing Partner wa Kampuni ya Sheria ya Afrika Legal Consultant, kwenye hii Wiki ya Sheria tumeamua sisi kwa udogo wetu tutatoa huduma hii kwa wana-Temeke," alisema.


CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30823 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

OLYMPIC PETROLEUM (T) LTD & 3 OTHERS ………………. ACCUSED PERSONS

**Summons to an Accused Person**
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: **Jibril Mohamud Omar, Director, Olympic Petroleum (T) Limited, Plot No. P28250, Segerea Area, Ilala Municipality, DSM City**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer a charge of **Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws**, you are hereby required to appear in person before this Court on the …04… day of …02… 2025

**Herein fail not.**

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this …10th… day of …JANUARY… 2025

Resident Magistrate

RESIDENT MAGISTRATE COURT KIVUKONI/KINONDONI, DAR ES SALAAM

183427



CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30823 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

OLYMPIC PETROLEUM (T) LTD & 3 OTHERS ………………. ACCUSED PERSONS

**Summons to an Accused Person**
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: **Ally Mohamud Adon, Director, Olympic Petroleum (T) Limited, Plot No. P28250, Segerea Area, Ilala Municipality, DSM City**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer a charge of **Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws**, you are hereby required to appear in person before this Court on the …04… day of …02… 2025

**Herein fail not.**

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this …10th… day of …JANUARY… 2025

Resident Magistrate

RESIDENT MAGISTRATE COURT KIVUKONI/KINONDONI, DAR ES SALAAM

183427

## RIPOTI MAALUMU -3

# Wadau watoa mbinu za kudhibiti taka za plastiki

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

**Sehemu ya pili ya ripoti hii jana iliangazia kiini cha mrundikano wa taka, zikiwamo za plastiki, zinazowaweka hatarini kiafya wakazi wa Manispaa ya Morogoro na maeneo jirani. Endelea na sehemu ya mwisho ya ripoti hii kupata undani wa mustakabali wake...**



Rundo la taka likiwa limetelekezwa baada ya kifaa maalumu cha kuhifadhi taka hizo kutozihimili kwenye eneo la Bwalo la Umwema, Manispaa ya Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"NCHI wanachama zinapaswa kuwa na mifumo bora ya usimamizi wa mazingira inayochangia ustawi wa jamii na kiuchumi kwa watu katika eneo husika."

Hili ni lengo kuu la Azimio la Usimamizi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Azimio hili liliridhiwa na nchi wanachama wa jumuiya hiyo Agosti 18, 2014 wakati wa Mkutano wa 34 wa Wakuu wa Serikali na Nchi Wanachama uliofanyika Zimbabwe.

Hata hivyo, kinachoshuhudiwa katika Manispaa ya Morogoro, hasa katika eneo hili la kutokuwa na mifumo bora ya udhibiti wa taka mitaani, kinakinzana na maelekezo ya azimio hilo SADC la miaka 10 iliyopita. Tanzania ni mwanachama mwasisi wa SADC.

Kukabiliana na mrundikano wa taka, zikiwamo za plastiki katika manispaa hiyo, Balozi wa Mazingira nchini, Chage Chage anasema wadau wa mazingira wanapaswa kutoa elimu kwa jamii ili itambue madhara ya taka hizo.

Vilevile, Chage anashauri watendaji wa serikali katika manispaa hiyo wasimamie Sheria ya Mazingira na kanuni zake kuhakikisha inatekelezwa ipasavyo.

"Mamlaka zilizopewa jukumu la kusimamia sheria hii zikitimiza wajibu wake vizuri na elimu ya mazingira ikatolewa kwa wananchi, Manispaa ya Morogoro inaweza kuwa ya mfano kwa usafi nchini," Chage anasema.

Balozi huyo anayetambuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, anasema maeneo mengi katika manispaa hiyo hayana vifaa vya kuhifadhi taka na hivyo watu wamekuwa wanatupa ovyo taka, hasa chupa cha plastiki baada ya kuzitumia, hata kuchangia uharibifu wa mazingira.

Chage pia anashauri manispaa hiyo kuweka mifumo ya urejelezaji taka, akiwa na ufafanuzi kuwa: "Baadhi ya taka, zikiwamo za plastiki, zikifanyiwa urejeleshaji, huzalisha bidhaa nyingine kwa ajili ya matumizi. Taka hizo zikifanyiwa urejeleshaji, zinakuwa mbolea.

"Shughuli za urejeleshaji taka hizi zinafungua fursa kwa wananchi kujiajiri kupitia ukusanyaji taka, hasa za plastiki. Hapo sasa mbali na kuweka mji huu kuwa safi, pia kunachochea maendeleo ya kiuchumi.

"Niwapongeze wale wote walioamua kujiajiri kwa kuokota taka za plastiki katika Manispaa ya Morogoro kwani wanachangia sana kuweka mji katika mazingira mazuri. Wananchi wawape ushirikiano mzuri badala ya kuwatazama kama ni wahalifu."

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Clement Lubeya anasema taka ni kisababishi ya uchafuzi wa mazingira, hivyo ni muhimu wananchi kupewa elimu ya kuepukana na uchafuzi wa mazingira ikiwa ni pamoja na utupaji ovyo wa taka.

Bingwa huyo pia anashauri manispaa kuweka vifaa kwa ajili ya kutenganisha taka mitaani.

"Bila elimu ya usafi wa mazingira, wananchi wataendelea kutupa ovyo taka, watarundika taka hizo sehemu moja. Elimu thabiti ikitolewa, wananchi watakuwa na uelewa. Ndiyo watakuwa wa kwanza kuhakikisha mazingira yanalindwa dhidi ya uchafu," Dk. Lubeya anashauri.

Daktari wa Mifugo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Esron Karimuribo, anashauri serikali kuweka mfumo wa urejelezaji taka, hasa za plastiki, akiamini hatua hiyo itasaidia kutaongeza kasi ya ukusanyaji taka hizo mitaani tofauti na ilivyo hivi sasa.

Sarah Pima, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), anaunga mkono hoja ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya taka, akieleza kuwa jamii ikiwa na uelewa mzuri wa athari za taka, itakuwa mstari wa mbele kutunza mazingira.

Anasema taasisi yake inayojishughulisha na mazingira kuhakikisha kunakuwa na mazingira safi na salama hivi sasa inatekeleza Mradi wa Uwajibikaji wa Wazalishaji Taka (EPR) ambao pamoja na mambo mengine, unalenga kuwajengea uelewa wadau mbalimbali wa mazingira, wakiwamo waokota taka za plastiki.

"Sheria ya Mazingira ipo lakini haitekelezwi ipasavyo hususani kwa wafanyabiashara wakubwa wanaozalisha hizo taka za plastiki. HUDEFO tunatamani kuona kila anayekwenda kinyume cha sera na sheria anawajibishwa," anasema. Mkurugenzi Sarah anashauri kuwe na utaratibu mzuri wa kisheria unaowalazimisha wazalishaji bidhaa zote za plastiki kununua chupa za plastiki zilizotumika na kuzichakata upya ili zingie tena sokoni.

Anasema kuwa wao HUDEFO wanaamini kuwa kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuondoa taka ngumu mitaani, pia kutoa fursa nyingi za kuichumi kwa waokota chupa, ikiwamo katika Mji wa Morogoro kunakolalamikiwa kuwa na mrundikano wa taka hizo.

Ally Juma ni mwokotaji chupa za plastiki mjini Morogoro. Analalama wamekuwa wanakabiliwa na changamoto nyingi katika shughuli zao kutokana na jamii kuwa na mtazamo hasi dhidi yao, hata baadhi yao kuuawa kwa kipigo wakidhaniwa ni wezi.

Mkazi huyo wa mtaa wa Nanenane, kata ya Tungi, anasema: "Siku moja niliamka alfajiri kwenda kuokota chupa za plastiki. Siku hiyo kamwe sitoisahau maishani mwangu kwani nilikumbana na kipigo kikali nikidhaniwa ni mwizi.

"Wakati ninaokota chupa, kulipigwa yowe la "mwizi... mwizi... mwizi... Nilipigwa sana, wakati wanaendelea kunishambulia kwa kipigo, walitokea wasamalia wema walikuwa wanakwenda kazini ambao walikuwa wananifahamu vizuri, hiyo ndiyo ikawa kunusurika kwangu."

Huku akimwonesha makovu ya kichwani yaliyotokana na kipigo hicho, Juma anaomba jamii iwatambue na kuwathamini waokotaji chupa za plastiki kwa kuwa wanasaidia kutunza mazingira.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***


CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30823 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

OLYMPIC PETROLEUM (T) LTD & 3 OTHERS .................... ACCUSED PERSONS

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: **Ibrahim Mohamud Odon, Director, Olympic Petroleum (T) Limited, Plot No. P28250, Segerea Area, Ilala Municipality, DSM City**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer a charge of **Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws**, you are hereby required to appear in person before this Court on the ......04...... day of ......02...... 2025

**Herein fail not.**

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this ......10...... day of ......01...... 2025

Resident Magistrate

183427



## Wafanyabiashara walalamikia utitiri wa kodi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BAADHI ya wafanyabiashara mkoani hapa, wameiomba serikali kupunguza utitiri wa kodi wanazotozwa na halmashauri ili kunuia uchumi wao na kulinda mitaji.

Wakitoa maoni yao jana jijini Arusha, mbele ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi nchini, wafanyabiashara hao, walidai kuwa utiriri wa kodi hizo unaonyesha dhahiri kuwa thamani yao ni ndogo kama Watanzania.

Wafanyabiashara hao, Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Kodi Kanda ya Kaskazini, Nicholaus Duhia na Adolf Locken, Mwenyekiti wa Chama cha Wasafirishaji wa Abiria Mkoa wa Arusha (AKIBOA), walisema hayo wakati wakiwasilisha maoni yao kwa tume hiyo kuhusu sheria ya kodi inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Walisema waliwasilisha maoni yao na kupendekeza kodi hiyo ishuke kutoka asilimia tatu hadi kufika 0.1 kulingana na huduma walizotoa.

Juliana Donald kutoka Umoja wa Wafanyabiashara Wanawake Arusha.

Juliana ameiomba TRA kuacha kuweka vizuizi vya kodi hasa eneo la Katesh wilayani Hanan'g Mkoa wa Manyara na kuondoa usumbufu kwa kuzuia magari yenye mizigo kuendelea na safari.

"TRA wanatukwaza hasa eneo la Katesh unapoagiza mzigo kutoka Singida kuja Arusha, ukifika eneo hilo unazuiliwa kupita sababu unadaiwa kodi sasa mnataka tufunge viwanda vyetu au kitu gani kama tunadaiwa basi tulipe kidogo kidogo na si kuzuia gari lenye mzigo," alisema.

Kwa upande mwingine, wafanyabiashara hao walilalamikia maeneo ya mipakani bidhaa zao kuzuiwa hadi miezi mitatu maeneo ya mipakani, hali inayoleta na kusababisha hasara.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue, aliwasihi wafanyabiashara hao kutoa mawazo yao ili kumsaidia Rais Samia Hassan Suluhu kuja na mpango mzuri wa ukusanyaji wa kodi nchini.

Balozi Sefue alimwagiza Katibu Tawala Msaidizi (Viwanda, Biashara na Uwekezaji) Mkoa Arusha, Frank Mmbando, kuhakikisha hakuna mtu yoyote atakayesumbuliwa katika utoaji wa maoni kwa kuwa tume hiyo imeundwa na Rais Samia kutatua kero za kodi nchini.

# Wanafunzi wasakwa kwa 'kukacha' kidato cha kwanza

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameagiza kusakwa kwa nusu ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa kutoripoti kwenye shule walizopangiwa ili waanze masomo mara moja.

Babu alitoa agizo hilo baada ya kupata taarifa ya wanafunzi hao kushindwa kuripoti kwenye shule za sekondari walizopangiwa mkoani humo hadi kufikia Januari 17, mwaka huu.

Wanafunzi hao na wengine walitakiwa kuripoti kwenye shule hizo Januari 13, mwaka huu baada ya kufunguliwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisa Elimu Taaluma wa mkoa huo, Abdalla Migila kuhusu hali ya elimu, mpaka kufikia Januari 17, mwaka huu wanafunzi 15,135 kati ya 31,039 sawa na asilimia 51, walikuwa hawajaripoti shuleni.

"Kwa kidato cha kwanza mwaka huu, tulitarajia waingie kwenye shule zetu wanafunzi 31,039, lakini mpaka tarehe 17 Januari tumeandikisha wanafunzi 15, 904 tu, ambao ni sawa na asilimia 51,"alisema Migila.

Kutokana na hali hiyo, Babu, amewaagiza wakuu wa wilaya zote mkoani humo kuhakikisha ndani ya siku saba wanafunzi hao wanasakwa na kuhakikisha wanaripoti shuleni.

Vilevile, aliwaagiza watendaji wa kata na vijiji vyote kufuatilia kwenye maeneo yao na kuhakikisha wanafunzi hao wanapatikana na kuanza masomo mara moja.

"Inasikitisha kuona idadi kubwa ya wanafunzi hadi sasa bado hawajaripoti shuleni na wako mtaani, jambo ambalo si sawa, hasa wakati huu ambao serikali imejenga miundombinu mingi ya shule na kuondoa ada.

"Watendaji wa kata, naamini mnafahamu kuwa sheria iko ya mzazi au mlezi ambaye mtoto wake hajaenda shule kuanza masomo, anakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Sasa mbona nyinyi hamuitumii sheria hii?" alihoji Babu.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kulia), akimlisha keki Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, wakati wa maadhimisho ya kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa ya Rais Samia Suluhu Hassan, wilayani Kiteto, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Virusi fungashada pasua kichwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wa tasnia ya migomba nchini wamejifungia kwa siku tano mjini hapa Mkoa wa Kilimanjaro, kuandaa rasimu ya mkakati na mpango kazi wa kutokomeza Virusi vya Fungashada la Migomba (BBTV) kwa kuathiri mavuno ya ndizi kwa asilimia 100.

Wadau hao ni pamoja na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), Shirika la Chakula Duniani (FAO) na mashirika wenza yanayopambana kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo.

Jana, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Afya ya Mimea wa TPHPA, Dk. Ben Ngowi, akizungumzia ugonjwa huo wa fungashada la migomba, alisema BBTV imesambaa ukanda wa kaskazini mashariki, nyanda za juu kusini, ziwa na magharibi, ambako ndizi ni zao kuu la chakula na biashara.

Dk. Ngowi, alisema wakati sasa wa kuja na mkakati kama jamii, wadau wa maendeleo, wadhibiti ubora na TPHPA.

Alisema baada ya mkakati huo, watapeleka kwa wananchi ili ufanyiwe tathmini na kurekebisha penye mapungufu.

"Nia ni kuji-committ (kujifunga) kupitia sheria ndogo za vijiji ili kuudhibiti ugonjwa huu, na hasa usafirishaji wa mbegu kutoka eneo moja kwenda jingine," alisema Dk. Ngowi na kuongeza kuwa:

"Ugonjwa huu wa BBTV, unaweza ukaondoa kabisa mavuno kwa asilimia 100, na matokeo tumeanza kuyaona kule Wilaya ya Buhigwe, Kigoma, na umesababisha tuunde mkakati wa makusudi wa kufidia kile tulichopotea kutokana na uharibifu."

Alisema TPHPA inafanya juhudi kudhibiti ugonjwa huo kupitia Wizara ya Kilimo ili kurudisha hali ya kawaida na kujenga uelewa kwa wananchi, wakulima na wadau kwenye mnyororo wa thamani.


Kwa mujibu wa Dk. Ngowi, TPHPA na wadau hao, wamechukua hatua kudhibiti virusi hivyo kwa kung'oa au kuua migomba ambayo imeshambuliwa na virusi hivyo.

"Pia tunachoma sindano ambazo zina viuagugu ambavyo vinaenda kuua kabisa ule mmea wa mgomba," alisema Dk. Ngowi.

STREPHIT unatekelezwa na FAO na kufadhiliwa kwa makubaliano kati ya Serikali, Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Chakula Duniani (FAO).

Mshauri wa Kiufundi (Ulinzi wa Mimea) wa FAO, Dk. Monday Ahonsi, akieleza umuhimu wa kutokomeza virusi vya BBTV nchini, ubia na jukumu la STREPHIT katika mchakato huo, alisema kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), wamedhamiria kutokomeza ugonjwa huo nchini.

"Mpango huu unalenga kuimarisha huduma za afya ya mimea na kukuza upatikanaji wa mazao ya kilimo yaliyo salama, yenye ubora wa juu, ndani na nje ya nchi," alisema.





# Mv. Umoja kuanza kupeleka shehena ya chakula Sudan

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limesema litarejesha ushirikiano na Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) wa usafirishaji shehena ya chakula kutoka Bandari ya Dar es Salaam na Mwanza nchini kwenda Sudan ya Kusini baada ya kusitishwa mwaka 2019.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa WFP, Sala Maharenovic, aliyeambatana na wawakilishi wa shirika hilo kutoka makao makuu Roma nchini humo katika ziara yao makao makuu ya TASHICO jijini hapa.

Maharenovic, pamoja na mambo mengine, alisema ziara hiyo inalenga kufanya tathmini ya ushirikiano walioanzisha takribani miaka 10 iliyopita na kampuni hiyo ambayo awali ilikuwa ikijulikana Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL).

"Mazungumzo haya ni muhimu kupata tathmini ya kina ni mahitaji gani yanayohitajika sasa ili kuboresha zaidi mahusiano yetu WFP na TASHICO," alisema Maharenovic.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASHICO, Eric Hamissi, alisema ujio huo ni mwanzo wa kurejesha usafirishaji shehena ya mizigo kutoka kwao.

Hamissi, alisema Mv. Umoja ilisimama kufanya kazi mwaka 2019 na kwamba serikali ilitoa Sh.bilioni 19.5 mwaka 2021 kuifanya ukarabati na kurejea katika hali yake ya kawaida.

Alisema shirika hilo limekuwa wadau wakubwa wa usafirishaji wa shehena ya chakula kwa njia ya maji kwa kutumia Mv. Umoja kutoka Bandari ya Mwanza nchini kwenda Sudan ya Kusini kupitia Uganda.

"Nakumbuka wakati huo meli yetu kubwa ya mizigo ya Mv. Umoja ilikuwa ikifanya kazi kwa kusuasua, lakini tuliweza kupata shehena nyingi ya mizigo kutoka kwa wadau wetu," alisema Hamissi.

Mkuu wa Kitengo cha Usafirishaji na Ugavi wa WFP nchini, Mamoud Mabuyu, alisema tathmini wanayoifanya itakuja na mapendekezo juu ya nini kifanyike.

Ofisa Masoko Mkuu wa TASHICO, Eugenia Punjila, alisema WFP wamekuwa wakisafirisha shehena ya chakula na mahitaji mengine ya msaada kupitia meli hiyo kwenda Sudan ya Kusini kupitia Uganda.

Nahodha wa Mv. Umoja, Bembele Samson N'gwita, alisema kuna mabadiliko baada ya ukarabati mkubwa uliofanyika kwenye meli hiyo tofauti na ilivyokuwa miaka 10 iliyopita.




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (kushoto), akikabidhi moja kati ya pikipiki 15 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Solomon Shati, zilizotolewa na serikali kwa halmashauri za mkoa huo juzi, ili kusambaza chanjo kwa watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wiki ya Sheria yaanza kwa migogoro 1,300

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

ZAIDI ya migogoro 1,300 ya wananchi wa vijiji 270 mkoani Mara imepokelewa katika Kampeni ya Samia Legal Aid wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria nchini mwishoni mwa wiki iliyopita.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Evans Mtambi wakati akifungua maadhimisho hayo.

Mtambi, alisema wananchi hao 103,163 wamewasilisha malalamiko hayo baada ya kupata elimu ya msaada wa kisheria bure kupitia katika kampeni hiyo iliyoanza Desemba 11 hadi 20, mwaka jana mkoani hapa.

Alisema kati ya migogoro hiyo, 224 imetatatuliwa na wataalamu waliobobea katika sheria, huku mingine 1,079 ikiendelea kutafutiwa ufumbuzi.

"Hivyo sasa niwaombe mtumie vema wiki hii ya sheria kwa kujitokeza kwa wingi mje hapa uwanjani mpate msaada wa sheria bila malipo. Niwashukuru wadau wote mliofika hapa kwani mtakuwa msaada kwa wananchi," alisema Mtambi.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, Fahamu Mtulya, alisema mahakama hiyo imeboresha utendaji wake wa kazi kwa kutumia mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Jaji Mtulya, alisema tangu kuanza kutumika TEHAMA, wanapokea mashauri kwa njia ya kielektroniki bila mhusika kuwapo mahakamani na kurahisisha utoaji huduma.

Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Monica Onesmo, alisema kilele cha wiki hiyo, Februari 2, mwaka huu, watajiunga na wenzao wa Mkoa wa Mwanza kushiriki bonanza litakalofanyika Uwanja wa Nyamagana.

Monica, alisema bonanza hilo litajumuisha wafanyakazi wa mahakama kuu wa Mara, Mwanza na Shinyanga likiwa na kauli mbiu isemayo 'Tanzania ya 2050 Nafasi ya Taasisi zinazosimamia Haki Madai katika kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo'.

## Kamati ya Bunge yapongeza utendaji wa Barrick, Twiga

**Na Faustine Feliciane**

MWENYEKITI wa Kamati ya Bunge ya Madini, Kilumbe N'genda, ameipongeza serikali kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na uwazi katika sekta ya madini nchini.

Akizungumza wakati wa kikao cha kupokea ripoti ya utendaji kazi wa Kampuni ya Barrick na ile ya Serikali ya Twiga, Ng'enda, alisema moja ya vitu ambavyo kamati yake imekuwa ikipigia kelele ni uwazi kwenye utendaji wa makampuni hayo yenye ubia.

"Niwapongeza Barrick pamoja na kampuni ya serikali ya Twiga Mineral Corporation kwa kuweka uwazi wa utendaji wenu na kutoa taarifa ya kile mlichokifanya katika kila kipindi cha robo mwaka, na sisi kamati tumekuwa tukipiga kelele sana kwa makampuni mengine yenye ubia na serikali kufanya hivi, kwa kweli tunawapongeza sana," alisema.

Alisema eneo lingine ambalo wao kama kamati wameona kuna mabadiliko ni pamoja na kuweka mahusiano mazuri kati ya wananchi na wawekezaji kwenye maeneo ya uchimbaji madini.

"Kwa sasa tunashuhudia migogoro mingi kati ya wananchi na migodi imepungua kwa kiasi kikubwa sana, ni jambo zuri na kamati tumeona juhudi za pamoja zinazofanywa na mwekezaji na serikali katika kutafuta maelewano na wananchi," alisema Ng'enda ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini.

Alisema kipekee anaipongeza ya Barrick kwa kutoa kipaumbele kwa watanzania kushika nafasi za juu kwenye migodi yake ya Bulyanhulu na North Mara.

"Kwenye taarifa tumeambiwa asilimia 96 ya wafanyakazi wa migodi hii ni Watanzania, tunapongeza kwa kuwajali wazawa na ni jambo lenye faida kwa taifa," alisema.

Awali akiwasilisha ripoti robo ya mwisho ya mwaka jana, Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Brsitow, alisema asilimia 57 ya wafanyakazi viongozi katika migodi ya Bulynahulu na North Mara ni Watanzania.

"Barrick imeajili wafanyakazi 5,933 ambao wote ni Watanzania sawa na asilimia 96 ya wafanyakazi wote huku wafanyakazi 252 pekee sawa na asilimia nne kutoka nje, tunajivunia kutoa fursa kwa watanzania katika kuendesha migodi hii," alisema Bristow.



Ukurasa 12

## TAKUKURU Tarime si shwari, ni madai kuanza kampeni, kugawa rushwa

DR MISSION 300



Ukurasa 13

## Afrika si ya kukosa umeme, imesheheni vyanzo vyote



Ukurasa 14

## IBRAHIM TRAORÉ
## Anayevutia mamilioni ya vijana Afrika, Bongo walimtamani, lakini hakutokea



MBOWE ALIPOSTAAFISHWA

# Hoja tusibadili jenerali katikati ya vita ilivyomtoa ulingoni, kumwinua Lissu

**Na Halfani Chusi**

MBIO za uchaguzi CHADEMA, zimefikia ukingoni Tundu Lissu ndiye Mwenyekiti Taifa na sasa anapanda daraja kutoka makamu na kuwa mwenyekiti, ni baada ya kumbwaga Freeman Mbowe.

Kilichokonga hisia za wafuasi na wajumbe waliopiga kura, ni namna Lissu alivyopangua hoja ya Mbowe anayesisitiza 'hakuna sababu ya kubadilisha jenerali mzoefu, katikati ya mapambano.'

Ukumbini wakati wa kunadi sera wajumbe walielekea kumkubali Mbowe na hata kumpigia makofi japo haikuruhusiwa kushangilia huku wengine wakiamini Lissu, aliyezungumza wa mwisho asingekuwa na jipya.

Katika sera zake kwa wajumbe Mbowe anajinadi akiwataka wasibadilishe jenerali anayeongoza mapambano vitani wakati chama kipo katikati ya vita, na kwamba kufanya hivyo ni hatari kwa ustawi wa CHADEMA.

Anawaambia wanahitaji jenerali mzoefu akiwataka wasidanganyike kwa kuwa uzoefu ni muhimu kukuza taasisi.

"Tusifanye mchezo wa kupima ukali wa sumu kwa kuionja, kutokana na kazi kubwa niliyoifanya na wote mnatambua hilo. Nimebuni mikakati, ninapolifuatilia jambo nalifuatilia kwa kina kwa sababu nakipenda chama.

"Ninakiona kama lulu ya taifa. Nendeni na mtu aliyepimika, kuzoeleka kwa mikakati na utayari wa kumsaidia mwingine. Ninaomba mniamini sitawaangusha kama ambavyo sijawahi kwa kujenga chama hiki kwa miaka 20," anasema akioomba kura.

Shangwe zikaibuka, mjumbe akahoji iwapo ni kosa kubadili jenerali wakati wa vita, si sahihi kuibadili CCM wakati huu?



Sura za Freeman Mbowe na Tundu Lissu, katika uchaguzi wa CHADEMA. **PICHA: HALFAN CHUSI**

Mbowe akajibu, kisha akawaamsha wajumbe wakisema 'anatosha kuendelea na nafasi hiyo'."

### LISU ULINGONI

Anaanza kukosoa hoja ya kutokimbilia kubadili jenerali katikati ya vita, akiwakumbusha madhila ambayo chama hicho kimepitia katika uchaguzi wa 2019, 2020 na 2024.

Lissu mwanasheria mbobezi anasema: "Mwaka 2020, CHADEMA iliambulia mbunge mmoja wa jimbo wa kuchaguliwa na wananchi, katika uchaguzi mkuu na miezi miwili iliyopita imeambulia asilimia 0.8 ya mitaa na vijiji kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, lakini jenerali yupo na hajafanya lolote kunusuru chama chake".

Ni kauli iliwafanya wajumbe kushindwa kuficha hisia zao, baadhi wakicheka, wengine wakimshangilia Lissu na baadhi wakilaumu wasimamizi wa uchaguzi kwa kufumbia macho 'mashambulizi' ya Lissu kwa Mbowe.

Lissu anahitimisha kwa kuwapa tahadhari wajumbe kwamba kwa kuzingatia mifano hiyo, walipaswa kuamua wamwongeze muda Mbowe aongoze kwa miaka 26 waendelee na madhila yaliyopo au wafanye mabadiliko kwa kumpa kura zao.

Kabla ya kupigakura, unafanyika uhakiki mkali wa wajumbe na kwa kipindi chote cha uchaguzi, wasimamizi wakihakikisha unakuwa wazi, wajumbe wakiitwa kwa majina (wasiozidi sita) kwenda kupiga kura kwa kupeana nafasi na kutolewa fursa kwa yeyote mwenye dukuduku au kuwa na taarifa yenye shaka, kuieleza na utatuzi na ufafanuzi kutolewa.

Ni hatua inayoibua wajumbe wachache ambao kikatiba hawakutakiwa kupiga kura hiyo taarifa ikatolewa na wakaondolewa ukumbini.

### WAFURAHISHWA

Baadhi ya wajumbe wa uchaguzi huo, wanapongeza utaratibu hasa uwazi na kushuhudiwa na kila mtu aliyekuwa ndani na nje ya ukumbi.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, anampongeza Lissu kwa ushindi na kumwahidi ushirikiano wa dhati katika harakati za kuimarisha demokrasia.

Ni katika mtandao wa X zamani (tweeter), Dorothy, anaandika: "Ninakupongeza Tundu Lissu kwa kushinda uchaguzi na kuwa mwenyekiti wa chama chako cha CHADEMA.

Kuchaguliwa kwako kunakufanya pia uwe Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD). Nikiwa makamu wako, ninakukaribisha sana katika uongozi wa TCD.

"Ninakuhakikishia ushirikiano wa dhati katika kupigania demokrasia ya nchi yetu. Pia ninampongeza Mbowe kwa kukamilisha muda wake wa uongozi na kuonesha mfano wa ukomavu wa kisiasa."

Kiongozi mstaafu ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, anamkaribisha Mbowe katika maisha mapya ya kustaafu huku akimpongeza kwa mchango wake alioutoa kwenye siasa za mageuzi.

"Ninakukaribisha mwenyekiti mstaafu katika ustaafu na kukuhakikishia kuwa kuna mengi ya kufanya nje ya siasa za uongozi katika kazi kubwa iliyo mbele yetu ya kujenga na kustawisha demokrasia inatuhitaji wanamageuzi walio ndani na nje ya uongozi."

### HALI ILIVYOKUWA

Ulinzi kuhakikisha hakuna hujuma katika uchaguzi huo uliimarika kila kona ya ukumbi hadi vyooni. Vyooni na ukumbini walinzi walitanda wakizuia wanachama kuzungumza kwa makundi au kuteta jambo lolote.

Walifanya hivyo kudhibiti uwezekano wa kutoa na kupokea rushwa kutokana na tuhuma zilizokikumba chama hicho siku za hivi karibuni zikidai kuna baadhi ya wanachama walipeana mlungula katika mazingira kama hayo.

INAENDELEA UK. 14

# TAKUKURU Tarime si shwari, ni madai kuanza kampeni, kugawa rushwa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

2025 ni mwaka wa uchaguzi wa madiwani, wabunge na marais wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar.

Ni msimu ambao utashuhudia wimbi la wengi kuanzia watumishi wa umma, wanataaluma na wafanyabiashara, wakijitosa kwenye harakati hizo.

Baadhi ya watumishi wa umma, wateule wa Rais, wanaonekana hawaridhiki na nafasi walizokabidhiwa wanataka pia wakawanie ubunge, ambao unawaweka kwenye nafasi nyingine za uteuzi, husussan uwaziri au unaibu, ukuu wa mikoa na ujumbe wa bodi.

**NI KIPI KIVUTIO?**

Zipo sababu nyingi zinazowafanya watumishi wa umma na wanataaluma kukimbilia kwenye ubunge, ikiwamo kuporomoka hadhi ya utumishi wa umma, kazi za kitaaluma maslahi madogo na hata hofu ya kutumbuliwa.

Pia kuchukuliwa kama njia rahisi ya kufikia mafanikio, uwanja wa kutoa michango ya kisiasa, uhaba wa mifumo ya taasisi huru na kutafuta fursa za kuteuliwa.

Wanaotamani ubunge si watumishi wa umma pekee wakiwamo wateule wa Rais, bali hata wanataaluma, wafanyakazi wa sekta binafsi na wafanyabiashara wanakimbilia ubunge.

Maslahi yatokanayo na ubunge ni jambo linalovutia wengi, siasa ikichukuliwa kuwa ni eneo linalolipa zaidi au lenye maslahi manono mno.

Takwimu zinaonyesha kuwa mbunge analipwa mshahara mnono kila mwezi, anapata posho kubwa ya kila kikao, akiongezewa na posho ya kujikimu kila siku achilia mbali safari, vikao vya kamati na kazi nyingine nyingi.

Anakusanya malipo hayo kwenye vikao vyote na kikubwa zaidi ni cha bajeti kinachoanza Aprili hadi Julai.

Ni heri kwake maana baada ya miaka mitano ya ubunge anapokea pensheni nono.

Mtu akichaguliwa kuwa mbunge anapata bima ya afya daraja la kwanza na familia yake, pia wana safari za nje lakini pia hana makato.

Maprofesa wanalipwa takribani Sh. 6,000,000 kwa mwezi lakini hawawafikii pensheni hiyo.

Kazi hiyo wanaweza kuifanya kwa miaka 30 lakini kuambulia pensheni wanayopata wabunge si jambo rahisi.

Pili, ni suala la demokrasia kila raia ana haki sawa kushiriki michakato ya kidemokrasia wakilindwa na katiba ya nchi inayosema kila mwananchi anayo haki ya kuchagua na kuchaguliwa kwa mujibu wa ibara ya 21 (1) na (2).

Jambo la tatu, wachambuzi wa masuala ya siasa wanasema, baadhi ya watiania wanapenda kuona mabadiliko ya kweli yanatokea nchini, ikitafsiriwa kukata tamaa pamoja na kuamua kushughulikia matatizo ya nchi kwa vitendo badala ya kusubiri wanasiasa pekee kila awamu.



Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara. **PICHA: MTANDAO**

> Hivi una ofisi yako uiache, unakuja na gari ya serikali unazurura jimboni unagawa rushwa. Sasa nilitarajia asimame hapa wote awape hela, si anagawa hela? Kwa hiyo apate taarifa...

Wachambuzi wa masuala ya siasa wanasema, ubunge ni ajira ya uhakika, ingawa ni kwa miaka mitano.

Nafasi za kuteuliwa si za kudumu na zinategemea mamlaka za uteuzi, kwani kuenguliwa ni kawaida, hivyo wengi wanaoteuliwa hawana uhakika na nafasi hizo kesho, ukiacha wale wanataaluma ambao wanatafuta maslahi.

Mbunge wa kuchaguliwa jimboni hawajibishwi na yeyote iwe amekaa kimya au kuzungumza bungeni, haiwezekani kutumbuliwa, labda baada ya miaka mitano mambo yamwendee kombo.

Mwalimu mkuu akipoboronga kwenye mitihani miaka miwili, anaweza kuhamishwa kwa adhabu kwenda vijijini.

Hakuna atakayemjali akihamishiwa mazingira mabaya, kadhalika halmashauri ikiboronga kwenye makusanyo ya maduhuli (mauzo na mapato), mhasibu au mkurugenzi anaweza kushushwa cheo hata kuhamishwa au kutimuliwa.

Mtu kama huyo anapopata nafasi ya kuwania ubunge anaona bora aende huko.

**RUSHWA INAJIPENYEZA**

Kwa kutambua 'vibunda vinono' kwenye ubunge, wengine huanza mapema kujisafishia njia wakitengeneza mazingira kwa wananchi, hususan wanachama wa vyama vya siasa.

Mathalani zipo taarifa kwamba, licha ya kwamba muda wa kampeni bado, wapo watu wanaoendelea na harakati za kujipenyeza majimboni.

Watiania wengi, kwa kutambua kwamba ubunge ni ajira na ina mapato makubwa, baadhi wako tayari kutumia fedha nyingi kwa kuwahonga wajumbe ili kupata nafasi hizo muhimu.

Kuna malalamiko kutoka mbunge wa jimbo la Tarime Vijijini Mwita Waitara, aliyedai kuna kigogo anazurura jimboni akitumia gari la serikali na kugawa rushwa kwa baadhi ya walengwa hususan wahusika vikao vya maamuzi.

Waitara anamtuhumu kuwa amekimbia ofisi yake na kuhamia jimboni kuwarubuni wajumbe ili kumpigia kura za maoni akiwapa fulana, kofia na 10,000 au 20,000.

Mbunge huyo anayataja maeneo kigogo huyo anayodaiwa kugawa posho, akisema atawataja hadharani waliopokea rushwa na maeneo yaliyotumika.

Anamtuhumu kigogo huyo bila kumtaja kwamba ameacha ofisi ya umma na kukimbilia jimboni kugawa takrima ili kununua wajumbe.

Aidha, anamtishia kuwa hatamvumilia na kuwatuma washirika wake kumfikishia salamu.

"...Huu ndio mgawanyo wa madaraka, mwingine atakuwa mtumishi wa umma, mwingine mfanyabiashara, atakuwapo pia mwanasiasa. Mimi siasa ni kazi yangu. Kama kuna mtu ataacha nyumba yake na kugawa tisheti, kofia na elfu 10..."

"Desemba 27, 2024 walikuwa wanagawana hela Sirari. Najua. Wakatoka hapo wakaenda kugawa Nyang'ungu na Gogona pale Masanga, ishirini ishirini kwenye bahasha. Desemba 26, waliitwa watu wa Ganyange, Binagi, wakaitwa watu wa Nyakonga, walienda polisi wakagawana 30,000 thelathini."

Anaongeza: "Nataka niwaambie. Mimi siyo mjinga, siwezi kusafisha nyumba aje mtu arukeruke hapa, ama zako ama zangu. Tutagawana mbao, nawaambia. Wale wote ambao walipokea rushwa nitawataja hadharani. Na shughuli hii imeanza."

Anasisitiza kuwa mtumishi huyo abake ofisini kwake ache kutangatanga, abaki njia kuu.

"Hivi una ofisi yako uiache, unakuja na gari ya serikali unazurura jimboni unagawa rushwa. Sasa nilitarajia asimame hapa wote awape hela, si anagawa hela? Kwa hiyo apate taarifa..."

**TAKUKURU IINGIE**

Kwa muktadha huo, wengi wanaishauri Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ikaingia mitaani kuwashughulikia wanaomwaga fedha kusaka ubunge na udiwani.

Na kwa kuanzia iwe Jimbo la Tarime Vijijini ambalo tayari kumeshatajwa kuwapo kwa vitendo hivyo vya rushwa.

Suala hapa si tu kumfuatilia kigogo anayemwaga fedha, lakini hata wengine pia, akiwamo mbunge mwenyewe, kwani naye ni mmoja wa watu wanaowania jimbo hilo.

Malalamiko hayo siyo za kuomba 'huruma' kutoka kwa mamlaka lakini zinaweza pia kuwa ni za kuzidiwa kete katika kugawa mlungula.

Hili la Tarime Vijijini liwe mwanzo kwa TAKUKURU kufanya ufuatiliaji majimboni na kata kukomesha rushwa na kuepusha jamii kuchagua viongozi wasio waadilifu ambao hawawezi kuleta maendeleo kwani watakuwa wanatafuta fursa ya kurejesha fedha zao na kuchuma nyingine.

TAKUKURU ina ofisi kila kona kwa hiyo siyo kazi ngumu kufanya ufuatiliaji ikiwa tu maofisa wataacha 'kukaa ofisini kula kiyoyozi'.

## DAR MISSION 300




Baadhi ya wajumbe wa Mkutano wa Nishati Afrika uliomalizika Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Afrika si ya kukosa umeme, imesheheni vyanzo vyote

**Na Gaudensia Mngumi**

MKUTANO wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika 'Mission 300', unaomalizika Dar es Salaam wiki hii unafanyika wakati matarajio ya kuzalisha umeme katika Mradi wa Afrika wa Bwawa la Inga lililoko DRC yakiwa bado kitendawili.

Ukipewa jina la Grand Inga Project, ndani ya Mto Kongo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, unatajwa kuwa ni mradi mkubwa duniani wa kuzalisha umeme wa maji wa megawati 44,000.

Iwapo ungekamilika ungeweza kutosha kufikisha nishati hiyo sehemu kubwa ya Afrika Kusini ya Sahara. Unakadiriwa kuwa gharama yake ni karibu dola bilioni 80 takribani Sh. trilioni 20.

FAIDA

Kwa mujibu wa BBC, unakadiriwa kuwa mradi mkubwa zaidi wa umeme wa maji duniani, wenye uwezo wa kuzalisha umeme mwingi zaidi kuliko Bwawa la Three Gorges la China.

Awali ulikuwa unafadhiliwa na Benki ya Dunia, ya Uwekezaji ya Ulaya na ya Maendeleo ya Afrika, ambazo zilihusika katika gharama za upembuzi yakinifu na tathmini za athari za mazingira, BBC inaongeza.

Hata hivyo kuna utata na kuna wasiwasi kuwa athari zinazoweza kujitokeza katika mazingira za mradi, ardhi, fidia na kama kuna manufaa yatapatikana kwa wawekezaji wa kigeni badala ya wakazi wa ndani.

Wakati mkutano wa 'Mission 300' ukiendelea kuandaa na kutoa Azimio la Nishati la Dar Es Salaam ni wazi kuwa kama mradi huo ungefanikiwa ungeweza kutoa msukumo mkubwa wa upatikanaji wa umeme kote Afrika na kuleta maendeleo hasa vijijini ambako huko ni giza.

Mkwamo wa Inga Dam, unaelezwa kuwa unatokana na kutokuelewana kuhusu uwazi kati ya serikali ya DRC na Benki ya Dunia mambo yanayochelewesha mradi huo kwa zaidi ya muongo mmoja.

Lakini kikubwa ni kupata ufadhili unaohitajika wa dola bilioni 80, hasa wakati huu ambao mahitaji ya umeme ni makubwa lakini upatikanaji ni changamoto.

Mtandao wa International Energy Agency, unasema matumizi ya umeme yameongezeka walakini, Afrika bado ilikuwa na karibu watu milioni 600 wasio na umeme ni takwimu za 2020. Aidha karibu Waafrika bilioni moja hawana nishati safi ya kupikia.

Mtandao wa The Global Economy, unasema kuwa mahitaji ya umeme Afrika ni kilowati milioni 4.76 ili kuzilisha nchi 53 za bara hilo, utafiti wa mwaka 2022.

Hata hivyo kukwama kwa juhudi za Inga Dam si jambo la kukatisha tamaa kwa sababu Afrika ni tajiri namba moja wa vyanzo vya nishati duniani.

**LIPO JUA**

Afrika ina vyanzo vingi vya umeme kuanzia jua kali la mwaka mzima, makaa ya mawe, gesi asilia, maji, upepo, geothermal au joto ardhi na pia madini ya nyuklia.

Uhaba wa umeme Afrika ni jambo ambalo linahitaji wataalamu na viongozi wake kuliona kuwa halikubaliki kwa sababu kwanza uwepo wa wingi wa jua kali ni suluhisho.

Kwa mfano kugusa vyanzo vichache kama jua na makaa ya mawe kunaweza kuleta mafanikio makubwa wakati Inga inakwama.

Ikumbukwe ni bara linalowaka jua mwaka mzima inakuwaje lisitumie sola au nishati jua?

Januari hii jua ni kali kote Afrika maeneo mengi yana viwango vya juu sana vya mwanga wa juakali na mionzi ya 'Ultra Violet' ni mingi ikichangia kuleta athari. Kuna karibu saa saba mpaka tisa za siku yenye jua kali likichoma Waafrika.

Kutokana na Afrika kuwa mojawapo ya mabara yenye jua huku sehemu kubwa ikipokea viwango vya juu vya mionzi ya jua, kiwe chanzo kikuu kitumiwe.

Uwepo wa jua kali mwaka mzima uwe kichocheo cha kuwa na umeme wa kutosha, Mission 300 ianze na jua kuongeza ubunifu na ugunduzi ili watu milioni 600 wanufaike na chanzo hicho ambacho kimejaa kila kona.

Tanzania, Uganda, Misri, Chad, Niger, Sudan, Sudan Kusini, Kenya na Madagascar kwa ujumla ukanda mzima wa Sahel na Sahara umejaa jua na huo uwe mkakati wa Afrika wa kuwa na umeme wa uhakika badala ya kujiingiza kwenye miradi ya gharama kubwa inayoongeza deni lake kutoka taasisi za fedha.

Lakini wakati tunatarajia kusoma Azimio la Nishati la Dar es Salaam litakalotolewa na 'Mission 300' Afrika isiache kutumia vyanzo vyote vya nishati ambavyo vilileta mapinduzi ya viwanda na maendeleo katika nchi tajiri na zilizoendelea.

Afrika iwekeze kwenye utaalamu, ubunifu na mbinu za kisasa kutumia madini ya urani kuzalisha umeme. Mbona Marekani na nchi nyingine zinatumia vinu vya urani kuzalisha umeme, Afrika inakwama wapi?

Taarifa za kimtandao zinaeleza kuwa Marekani inatumia umeme wa nyuklia, ikizalisha karibu asilimia 20 ya umeme wa nchi hiyo na kuifanya kuwa mzalishaji mkubwa zaidi wa nishati ya nyuklia duniani, Afrika kwanini ishindwe? Wataalamu wapo watumike kufikia azma hiyo.

Afrika ishirikiane kutumia rasilimali zake kuzalisha umeme, mathalani Tanzania ina makaa ya mawe tani takribani tani bilioni 1.5.

> Kwa mfano kugusa vyanzo vichache kama jua na makaa ya mawe kunaweza kuleta mafanikio makubwa wakati Inga inakwama.

Madini hayo yako Ngaka mkoani Ruvuma, kuna Mchuchuma wilayani Ludewa na Kiwira kama kuna tani zaidi ya bilioni 1.5 kwanini Tanzania isiwe kitovu cha kuzalisha umeme wa makaa ya mawe Ukanda wa Kusini mwa Afrika?

Inakuwaje Zambia inasafirisha shaba ghafi kwa miaka 60 wakati kuna makaa ya mawe yanayoweza kuzalisha umeme na kuiyeyusha, kuichakata na kuiongezea thamani ili kupata faida zaidi?

Hata sasa kwanini Tanzania iendelee kuagiza chuma nje wakati kuna hifadhi ya chuma cha kutosha Liganga?

Kinachohitajika sasa ni kanda za kiuchumi kama SADC, COMESA na EAC, kuungana na kuanzisha miradi ya kuzalisha umeme mfano wa makaa ya mawe ili chuma kutoka Mchuchuma na Shaba ya Zambia ziyeyushwe na kuuzwa zikiwa na thamani zaidi.

Pia vyuma (ingots) vitumiwe kuunda bidhaa kama mabati, magari, reli na meli hapa Afrika hata kuuzwa nje kwa faida.

Pamoja na kuwa na viwanda mradi huo uchangie kuwa na nishati kwenye gridi ya Afrika huku ukifua madini kama chuma na shaba na kusongesha mbele uchumi.

IBRAHIM TRAORÉ

# Anayevutia mamilioni ya vijana Afrika, Bongo walimtamani, lakini hakutokea

**Na Christina Mwakangale**

MWONEKANO wake na falsafa zake, kiongozi wa serikali ya kijeshi Burkina Faso, Kapteni Ibrahim Traoré, kumemjengea umaarufu si nchini mwake tu bali barani Afrika.

Wakati orodha ya washiriki wa nchi takribani 24 ikitajwa kuwa washiriki wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliomalizika jana Dar es Salaam, akiwamo Traoré, mitandaoni kijana huyo amejiongezea umaarufu.

Kapteni Traoré (37), Oktoba, mwaka 2022 aliingia madarakani baada ya kufanyika mapinduzi na kuondoshwa ikulu Paul-Henri Sandaogo Damiba.

Muda mfupi, Traoré alitangaza katika televisheni ya taifa, amempindua madarakani kiongozi huyo wa kijeshi.

Kijana huyo ana falsafa zake ikiwamo kupinga anachodai Waafrika wamerithishwa na utawala wa kikoloni. Wiki chache zilizopita amepiga marufuku majaji wa nchi mwake kuvaa mawigi yenye mtindo wa kikoloni ya Ufaransa na Uingereza.

Vijana wanaojiita kizazi cha Gen Z, huko mitandaoni wanamtaja kama ndiye wamtakaye kulingana na wakati huu. Kiongozi huyo amesubiriwa kwa hamu kubwa kushiriki kwenye mkutano huo, Dar es Salaam, lakini hajaonekana.

Mitandaoni wengi wanaeleza nia yao ya kumwoana ana kwa ana, hasa mwonekano wa mavazi yake kijeshi akiwa na silaha yake muda wote.

Hivi karibuni pia anashika kasi mitandaoni baada ya nchi yake kulipa deni la nje lenye thamani ya dola bilioni 4.7 wakati huo huo akichukua udhibiti wa sekta ya madini ya dhahabu yenye faida kubwa nchini Burkina Faso.

Hatua hiyo imeibua hisia nyingi ndani na kimataifa, ikiashiria mabadiliko yanayoweza kutokea katika mtazamo wa Afrika wa uhuru wa kiuchumi na usimamizi wa rasilimali.



Rais Ibrahim Traore wa Burkina Faso. **PICHA: MTANDAO**

Baadhi ya maoni mtandaoni yalikuwa haya @BarakaMboyi anasema: "Mwamba kweli ni mzalendo Mwamba kweli ni mzalendo wa kweli kiukweli tumpe maua yake, viongozi wa Afrika waone mfano kwa Traoré.

**HISTORI ILIPOANZA**

Kapteni Traoré, Septemba 30, 2022, anamwondosha madarakani Luteni Damiba.

Awali, Damiba, anaanza kumwondoa Rais Roch Marc Christian Kabore, aliyeingia kwa kupindua pia.

Kapteni Traore, anaeleza sababu ya kuidhinisha mapinduzi hayo, ni kutokana na kushindwa kwa Luteni Damiba, kukabiliana na waasi.

Mbali na viongozi wa kijeshi, vipo vikosi vya wanamgambo, viongozi wa kimila na kidini, wakuu wa taasisi na wageni maalum wa rais wa mpito.

Mbele ya wajumbe wa Baraza la Katiba, Kapteni Ibrahim Traoré anainua mkono wake wa kulia na kuapa kwa heshima yake kuhifadhi, kuheshimu, kuheshimisha na kutetea katiba, makubaliano ya mpito na sheria.

Kufanya kila linalowezekana kuhakikisha haki kwa wakazi wote wa Burkina Faso.

**USALAMA KWANZA**

'Nitapigana hadi pumzi ya mwisho', anasema akihutubia wananchi wake bila kutumia karatasi zenye maandishi.

"Hakuna hasara kubwa itakayotokea kwa kuiondoa Burkina Faso katika hali hii. Dira yetu itakuwa watu daima. Kwa taifa langu, nitapigana hadi pumzi ya mwisho," anasema baada ya kula kiapo.

Anajitokeza sana katika vita dhidi ya waasi nchini Burkina Faso alikozaliwa kati ya 2019 na 2022. Alipandishwa cheo hadi kapteni mwaka wa 2020.

Muda mfupi baada ya kufanya mapinduzi dhidi ya utawala wa Damiba, Septemba 2022, Traore alikiri kwamba umri wake wa miaka 34 (wakati huo), ungekuwa mada ya mjadala kati ya wale wanaotilia shaka sifa zake za urais.

"Najua kwamba ni mdogo kuliko wengi wenu hapa. Hatukutaka kilichotokea (mapinduzi dhidi ya Damiba), lakini hatukuwa na chaguo," aliwaambia maaofisa wa serikali Oktoba 2022.

**MAVAZI**

Rais huyu huvaa mavazi ya kijeshi katika maonesho mengi ya umma.

Marais wenzake ambao mara nyingi huvalia suti zao za bei ghali, Traoré, mrefu zaidi huwa katika mwonekano wa kijeshi.

Akiwa na urefu wa zaidi ya futi sita, huvaa bareti nyekundu na glavu za kijivu. Katika uongozi wa kijeshi, Traore yuko katika cheo cha Captain, ni neno la Kifaransa. Kuna safu tatu juu ya ile ya kapteni, nao ni Luteni na Kanali.

Kwa kuwa koloni la zamani la Ufaransa, Burkina Faso ilipitisha muundo wa amri ya kijeshi ya Ufaransa.

Baada ya kuhudumu katika nyadhifa za chini katika jeshi la Burkina Faso, hatua kubwa ya Traoré ilikuja mwaka 2014, alipotumwa Mali kama mwanajeshi chini ya mpango wa Umoja wa Mataifa wa kulinda amani, MINUSMA.

Akiwa na umri wa miaka 26 wakati huo, Traoré alishinda "shambulio tata" la wanamgambo wenye itikadi kali katika eneo la kaskazini la Timbuktu, chanzo ambacho hakikutajwa jina kiliiambia Radio Omega.

"Tatizo ni kuona wakuu wa nchi za Kiafrika, ambao hawaleti chochote kwa watu wanaohangaika, wakiimba wimbo sawa na mabeberu wanaotuita 'wanamgambo'. Matokeo yake, wanaishia kututaja sisi kuwa watu wasioheshimu haki za binadamu," Traoré alisema.

"Sisi, wakuu wa nchi za Kiafrika, lazima tuache kutenda kama marimoti ambao wanacheza kila wakati mabeberu wanapovuta kamba zetu."

Alikwenda mbele kuwakashifu marais wa Afrika ambao "wanafurahi kupokea vitu na misaada ya bure." **BBC, DW, MITANDAO**

## Hoja tusibadili jenerali katikati ya vita ilivyomtoa ulingoni, kumwinua Lissu

**INATOKA UK. 11**

Baada ya Lissu, kutangazwa mshindi shangwe ikaibuka nje na ndani ya ukumbi huku wafuasi wake wakimuimba kwa kulitaja jina lake kumpongeza kwa ushindi.

Wenye mahaba na Mbowe wakapoa japo baada ya muda baada ya matokeo kutangazwa wakaanza kurejea katika hali ya kawaida na kwamba wako tayari kumuunga mkono mshindi.

Nje ya ukumbi wafuasi wa chama hicho, wakaikejeli timu Mbowe wakidai wamekula rushwa lakini wamemsaliti kwenye boksi wakimchagua Lissu.

Mmoja kati ya wafuasi hao akarusha kijembe, "wajumbe mmekula mpaka pilau na kuku lakini mmemchinja bosi wenu."

Nyimbo mbalimbali za chama hicho zikatawala ukumbi Mlimani City, vifijo na nderemo, ikawa burudani eneo nzima na kuvuta macho ya watazamaji kuanzia abiria wa daladala, wateja wa maduka ya Mlimani City na majirani.

Itakumbukwa ni uchaguzi uliofanyika usiku kucha ambapo wajumbe ndani ya ukumbi hawakupata hata dakika moja ya kulala kutokana na msuguano ulivyokuwa. Nje ya ukumbi wafuasi wa chama hicho wakifurika na wengine kulala pembezoni ya kuta za ukumbi hata sakafuni kwenye vibaraza.

Wapo wengine wakikesha kwa kupiga soga zinazoambatana na ubishi wa nani aneyeibuka mshindi na kwanini.

**SURA ZA USHINDI**

Punde baada ya kumaliza kuhesabu kura, wakala wa Lissu, Godbles Lema, akasambaza tabasamu na uso wenye bashasha, ikawa ishara kwa wafuasi kuwa matokeo ni mazuri, hivyo kulipuka kwa shangwe.

Aidha, wakala wa Mbowe, Boniface Jacob maarufu Boni Yai, akapoa baada ya kuhesabu kura, kabla ya matokeo kutangazwa, ndiyo ishara kwa timu Mbowe kwamba wameanguka.

**NJE YA UKUMBI**

Katibu wa CHADEMA Wilaya ya Kwamba Mkoa wa Mwanza, Samason Matobogolo, anasema uongozi mpya utaleta tija kwa sababu siasa za Mbowe zilizoeleka.

"Ninaona kuanzia kwenye matawi mpaka juu tutakuwa pamoja. Tutafanikiwa kuongeza wafuasi na chama chetu kitasonga zaidi," anasema Matobogolo.

Chama kimepata viongozi watakaowapeleka kupata mabadiliko, na ni uchaguzi wenye matokeo chanya kwa maslahi ya taifa, anaeleza.

Anasema wanachohitaji wanachama ni amani, umoja na upendo pamoja na kusimamia kile wanachokiamini ili kukuza imani kwa wanachama.



# Takwimu sensa zilivyonusuru upigaji Hanang'

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022 nchini, Anna Makinda, amesema takwimu zimeisaidia serikali kudhibiti udanganyifu katika janga la maporomoko ya matope yaliyotokea mwaka jana Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara mwaka jana.

"Kwa kutumia picha ya satelaiti zilisaidia kuonyesha majengo yote kwa uhalisia, unaweza ukapiga kijiji ukakichukua chote na kama isingekuwa hii sensa watu wangeipiga serikali pakubwa wangeweza kusema nilikuwa na nyumba ya mabati au ng'ombe 100 wakati mwingine inakuwa sio kweli," alisema Makinda wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wanachama wa Klabu za Waandishi wa Habari wa mikoa ya Dodoma na Singida yanafanyika mjini hapa kuhusu usambazaji na matumizi ya matokeo ya sensa hiyo tafiti nyingine.

Makinda ambaye ni Spika Mstaafu wa Bunge, alisema ubora wa sensa hiyo umethibitika na Umoja wa Mataifa (UN). Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022, Anna Makinda, amesema matokeo ya sensa hiyo yameisadia serikali kudhibiti udanganyifu ambao ungeisababishia kulipa mamilioni ya fedha kwa taarifa za udanganyifu katika janga la maporomoko ya matope lililotokea mwaka jana Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara mwaka jana.

Makinda ambaye ni Spika Mstaafu wa Bunge, alisema lengo la mafunzo haya ni kuvijengea uelewa vyombo vya habari ili viweze kutekeleza majukumu kikamilifu.

Alisema mafunzo hayo ni mfululizo wa yanayofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuanzia Septemba.

Hadi sasa klabu zote za waandishi wa habari nchini zimepewa mafunzo hayo muhimu kwa kuvijengea uwezo vyombo vya habari katika kutafsiri, kufanya uchambuzi na namna ya matumizi ya matokeo ya sensa.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema takwimu hizo za sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 zitasaidia kuondoa udanganyifu wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka huu.

"Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi kwa hiyo uwepo wa takwimu vizuri zitatusaidia hata kufanya uchaguzi wetu kwa amani na utulivu kwasababu tutakuwa tunaenda kitakwimu zaidi na ule udanganyifu mwingine ambao watu wamezoea kutudanganya tutakuwa tumeubaini," alisema.

Alisema vyombo vya habari vina umuhimu mkubwa duniani kote katika kuelimisha, kuburudisha na kuhabarisha, hivyo katika kuhakikisha matumizi ya takwimu za sensa yanafanikiwa ni muhimu vikatoa ushirikiano.

"Vyombo vya habari vimekuwa kiungo muhimu sana, lengo la serikali ni kuhakikisha matumizi ya sensa ya watu na makazi ili kuleta maendeleo haraka ya nchi," alisema.

## Ole Gabriel ashauri rushwa ipigwe vita nyumba za ibada

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama nchini, Profesa Elisante Ole Gabriel ameishauri Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) kutoa elimu ya rushwa kwa viongozi wa dini ili watumie nyumba zao za ibada kupiga vita vitendo hivyo katika jamii.

Prof. Elisante alitoa ushauri huo jana baada ya kutembelea Banda la TAKUKURU katika Maonesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea Viwanja vya Nyerere Square jijini hapa.

Alisema jamii ikihubiriwa kuwa na mwenendo mwema katika nyumba za ibada, itaisaidia kubadili tabia na kupunguza rushwa nchini.

"Nawashauri TAKUKURU elekezeni nguvu kuelimisha viongozi wa dini wasaidie kuielimisha jamii mapambano dhidi ya rushwa nchini," alisema.

Alisema viongozi hao wana sehemu kubwa ya kubadili jamii kuhusiana na vitendo viovu, hivyo elimu hiyo ya kupambana na rushwa ikielekezwa kwao, watasaidia kwa kiasi kikubwa kuelimisha na kupata mafanikio makubwa.

Kwa upande mwingine, aliipongeza taasisi hiyo kwa kazi kubwa wanayofanya kuielimisha jamii mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema taasisi hiyo, imekuwa ikigusa kila eneo kwa kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa na kusaidia kubadili fikra ya jamii baada ya kutambua madhara yake kwa kuanza kuepuka vitendo hivyo.

Anna Jackson, Mkazi wa Jiji la Dodoma, alisifu TAKUKURU kwa kuwa msaada kwa jamii kupata haki baada ya kupokea malalamiko yenye viashiria vya rushwa katika taasisi mbalimbali nchini.

"Nawapongeza TAKUKURU kwa msaada wanaotoa kwa jamii kupata haki ya madai na malalamiko," alisema Anna.

Kwa upande wake, Ofisa Uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Idda Siriwi, alisema wiki hiyo ya sheria wanaitumia kutoa elimu kwa wananchi dhidi ya rushwa nchini.

Idda, alisema elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ni muhimu kwa jamii kwa kuwa vitendo hivyo vinaathiri maendeleo ya wananchi na kuwanyima haki zao za msingi.



Askofu wa Kanisa la Baptist Tanzania, Kanda ya Kati, Anthony Mulyashimba (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Sheria cha Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Agnes Sayi, wakati wa Wiki ya Sheria 2025, katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma juzi. Katikati ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi mamlaka hiyo, Stanley Jackson. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Migogoro wakulima, wafugaji kuteka mkutano mkuu ALAT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) imepanga kutumia mkutano mkuu wa mwaka, kutafuta suluhu ya migogoro ya wakulima na wafugaji nchini kutokana na ukosefu wa malisho.

Migogoro hiyo imekuwa ikiibuka baadhi ya maeneo na kusababisha maafa ya watu, mifugo na uharibifu wa mazao.

Hivi karibuni matukio ya mapigano ya wakulima na wafugaji yameripotiwa katika baadhi ya mikoa ikiwamo Morogoro wilayani Kilosa, Tanga (Kilindi) na hifadhi za taifa baada ya wafugaji kudaiwa kuingiza mifugo kusaka malisho.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Murshid Ngeze, alisema maandalizi ya mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Februari 17 hadi 21, mwaka huu, jijini Mwanza, Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Ngeze, alisema katika mkutano huo, ajenga kubwa ambayo wamepanga kujadili na kutafutia suluhu ni kumaliza migogoro hiyo baina ya makundi hayo ambayo pia imekuwa ikisababisha uharibifu wa mali na mazao kwa kuliwa na mifugo kutokana na uhaba wa malisho.

"Kupitia mkutano huu tutajadili ni namna gani tunaweza kumaliza hali hii hata ikibidi kuandaa ziara ya kwenda nchini Botswana kuona ni namna gani wenzetu wanalima nyasi kwa ajili ya mifugo na kuondoa migogoro baini ya jamii hizo mbili," alisema.

Alisema kwa sasa migogoro hiyo nchini imekuwa ikiongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ongezeko la mifugo ambalo haliendani na idadi ya malisho.

Ngeze, aliitaja ajenda nyingine katika mkutano huo ni kuzikumbusha halmashauri nchini, kutekeleza maagizo ya serikali ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato.

Alisema agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Omary Mchengerwa kwenye mkutano Mkuu wa ALAT uliofanyika mwaka jana visiwani Zanzibar.

# Halmashauri kutumia bil.25/- kulipa madeni, maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** ITIGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida inatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 25 kulipa madeni kwa wazabuni, watumishi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha wa 2025/2026.

Bajeti hiyo ya Sh. bilioni 25.139 ilipitishwa jana na Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo baada ya kujadili makadirio ya mapato na kuridhia, itumike kwa mwaka huu unaonzia Juni mwaka huu kwa matumizi hayo.

Awali akiwasilisha bajeti hiyo, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Immanuel Dyelu, alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 17.334 zitatumika kwa matumizi ya kawaida ya halmashauri na Sh. bilioni 7.804 kutekeleza miradi ya maendeleo katika jamii.

Dyelu, alitaja vipaumbele vya halmashauri hiyo katika bajeti hiyo kuwa ni ujenzi wa maegesho ya kisasa katika eneo la Majengo, kituo cha mabasi, soko la kisasa eneo la Kata ya Tambukareli na kuanzisha mradi wa hewa ukaa.

Vipaumbele vingine ni kukamilisha ujenzi wa madarasa katika shule za msingi na sekondari, kulipa madeni ya wazabuni na watumishi, kununua gari la kukusanya taka ngumu na la Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hassan Simba, alisema hivi karibuni halmashauri inatarajia kusaini mkataba wa kufanya biashara ya hewa ya ukaa kama chanzo kipya cha kuiongeza mapato.

Mkurugenzi huyo, Ayoub Kambi, aliahidi halmashauri hiyo kusimamia kwa karibu ukusanyaji mapato ili fedha zitumike kutekeleza vipaumbele hivyo.





# RC aagiza uchunguzi sakata la wananchi kunyweshwa majitaka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeagiza kuundwa kwa kamati ya kuchunguza tatizo la wananchi wa Mtaa wa Lumbila katika Kata ya Iwambi jijini Mbeya kulalamika kuunganishiwa mfumo wa majitaka kwenye majisafi.

Pia, imewataka wananchi kutolihusisha tukio hilo na siasa huku ikiwatahadharisha baadhi ya wananchi wanaotaka kujinufaisha kiuchumi kutokana na tatizo hilo kwa kuanza kudai fedha kutoka katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya UWSA).

Juzi wakati wa sherehe ya kumbukizi ya kuzaliwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa kuunda kamati ya kuchunguza tatizo hilo ili hatua zichukuliwe.

Alisema kamati itakayoundwa ikikamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa hatua zitaanza kuchukuliwa dhidi ya watu wote watakaobainika kusababisha tatizo hilo pamoja na kuangalia namna ya kuwasaidia wananchi watakaokuwa wamedhurika.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo la Lumbila walisema tatizo hilo limetokea ni kwa mara ya pili ndani ya miaka miwili na kwamba linawaathiri kiafya.

Mmoja wa wananchi hao, Dorcas David aliomba Mbeya UWSA kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo ili lisitokee tena akidai kuwa linaathiri maisha yao na kuhatarisha afya zao.

"Tunaomba tatizo hili lipatiwe ufumbuzi wa kudumu, wamekuwa wakisingizia ujenzi wa barabara kwamba ndio unasababisha, sasa wahakikishe wanatafuta suluhu ya kudumu," alisema Dorcas.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-UWSA, Gilbert Kayange, aliwaomba radhi wananchi hao kutokana na tatizo hilo na akawahakikishia kuwa wameshaanza kuchukua hatua za kulitafutia ufumbuzi wa kudumu ili lisitoke tena.

Pia, aliwataka wananchi hao kufungulia maji muda wote ili yamwagike na kusafisha mabomba hayo kabla ya kuanza kuyatumia maji hayo huku akisisitiza kuwa mamlaka hiyo haitawatoza gharama yoyote.

Alisema kutokana na tatizo hilo mamlaka hiyo imewafutia wananchi wote wa eneo hilo ankara za maji kwa kipindi cha Januari ili kufidia hasara ambayo wananchi hao wameipata kutokana na uchafu wa maji hayo.

Wananchi wa eneo hilo walianza kulalamika kuwa wanatumia maji machafu tangu Januari 19, mwaka huu wakati ambao Jiji la Mbeya lilikuwa tayari limekumbwa na mlipuko wa kipindupindu.



Mafundi wa Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO), wakibadilisha nguzo kwa kuondoa za miti na kuweka za zege pamoja na transfoma yenye uwezo mkubwa, katika eneo la Miyomboni, mjini Iringa juzi, ili kuondoa tatizo la umeme. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mvua yaharibu ekari 138 za tumbaku

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MVUA iliyoambatana na mawe pamoja na upepo imeharibu ekari 138 za tumbaku katika Tarafa ya Kipembawe Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya.

Ofisa wa Bodi ya Tumbaku nchini (TTB), Loysujaki Kimiri alisema wakulima 31 wameathirika na mvua hiyo na kwamba kiwango cha uharibifu wa majani ya tumbaku ni wastani wa asilimia 22 kwa mashamba yote.

Kimiri alitoa taarifa hiyo jana wakati wa ziara ya Kamati ya Usalama ya Wilaya ambayo ilitembelea mashamba ya wakulima hao kwa lengo la kuona uharibifu na kujadili hatua za kuchukua ili kuwasaidia wakulima hao.

"Zilikuwapo ekari 298 ambazo wakulima hawa wameingia mkataba na kampuni mbalimbali na kati ya hizo zilizoathirika ni ekari 138 na tunaendelea kufanya tathmini zaidi," alisema Kimiri.

Aliongeza kuwa baada ya kupokea taarifa ya athari hizo walifanya ziara kwa wakulima hao na kutoa ushauri hatua iliyowapa matumaini baada ya kukata tamaa kutokana na hasara waliyopata.

Mmoja wa waathiriwa wa tukio hilo, Jema Jaluo, ambaye shamba lake la hekari 70 limeathirika kwa asilimia 50 alisema siku ya tukio mchana ulianza upepo mkali na kisha mvua iliyonyesha usiku ikiambatana na mawe.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mbarak Batenga aliwaelekeza wataalamu wa kilimo kuunda mfuko maalumu wa kusaidia wakulima wakati wa majanga ili kupunguza madhara yatokanayo na majanga hayo.

Alisema ameunda kamati ambayo itaandaa mwongozo wa namna ya kutengeneza mfuko wa majanga ambao wakulima watakuwa wanachangia kwa kukatwa asilimia ndogo, ili kusaidiana yanapotokea majanga hayo yanayosababisha hasara na kushindwa kulipa mkopo.

Alielekeza wataalamu hao kupitia vyama vya msingi vya ushirika na Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku (CHUTCU) kuweka utarabitu wa kuwa na mfuko maalumu wa majanga utakaosaidia yanapotokea majanga ili mkulima asipate hasara kwa asilimia 100.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Magunga, David Siwakwi, alisema zao hilo limekuwa chanzo kikuu cha kipato kwa wakulima katika kijiji chao na alipongeza mpango wa kuanzisha mfuko wa majanga na kuahidi kuunga mkono wazo hilo.

## RC azitwisha 'zigo' kamati za ulinzi vita ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Patrick Sawala ameziagiza kamati za ulinzi na usalama mkoani hapa kupambana na ukatili wa kijinsia katika maeneo yao kwa kuelimisha jamii kuachana na mila na desturi kandamizi.

Alitoa agizo hilo wakati akifungua mafunzo kwa watendaji wa kamati hizo kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji, mitaa, kata, wilaya na mkoa ya elimu ya uraia na utawala bora yanayotolewa na Wizara ya Katiba na Sheria na Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Alisema elimu hiyo itawasaidia kukabiliana na kukithiri kwa vitendo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya watu katika maeneo yao na kuiwezesha jamii kuishi kwa amani.

Alisema mafunzo hayo mkoani hapa yamekuja wakati mwafaka kwa watendaji hao, ikizingatiwa serikali kila kukicha inakemea vitendo hivyo ambavyo vimekuwa vikisababisha vifo kutokana na imani potofu.

Alisema watendaji hao kuanzia ngazi ya mkoa hadi vijiji watakwenda kutumia sheria walizojifunza kuwabaini wanaoshiriki vitendo hivyo dhidi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu na kuwachukulia hatua.

"Nawashukuru Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuendesha mafunzo haya kwa sababu yatazidi kupanua wigo kwa watendaji kufahamu sheria zitakazowasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao," alisema Sawala.

Pia, alizitaja baadhi ya changamoto zinazoikumba jamii katika utekelezaji wa majukumu yao na kukandamiza jamii kuwa ni mila na desturi.

Alisema anaamini watendaji watakwenda kuziondoa kwa kuwapa elimu wananchi waliyopapata kutoka wataalamu wa wizara hiyo.

Pia, aliwataka watendaji hao kwenda kubadilisha mtazamo wa jamii ili waachane na mila na desturi kandamizi kwa kujua haki zao za msingi.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mjini, Abdallah Mwaipaya, aliwasisitiza washiriki wa mafunzo hayo kwenda kufanya kazi kwa vitendo kwa manufaa ya jamii.

Mwaipaja alisema wao kama kamati ya ulinzi na usalama, miongoni mwa washiriki hao watakwenda kuwa mabalozi wazuri kwa wananchi kwa kutumia mafunzo hayo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Sheria kwa Umma wa Wizara hiyo, Abdurahmani Mshamu, alizitaja mada zinazotolewa katika mafunzo hayo kuwa ni pamoja na demokrasia na utawala bora, haki na wajibu wa jamii, madaraka kwa umma, ulinzi na usalama.

# TANGAZO

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITIES

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. In line with these expansion ambitions, ATCL invites applications from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

## 1. POSITION: FLIGHT OPERATIONS OFFICER II (5 POSTS)

### 1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS

- Must be a holder of Advanced level certificate of Secondary Education (Form VI)
- Must be a Holder of TCAA or other ICAO approved Flight Operations/Flight Dispatcher's License.
- Possession of Bachelor Degree will be an added advantage.

### 1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

i. Assisting the PIC in flight preparation and providing required information;
ii. Assisting the PIC in preparing the operational and ATS flight plans;
iii. Furnishing the PIC, while in flight, by appropriate means, with information which may be necessary for the safe conduct of the flight;
iv. In the event of an emergency, initiating the applicable procedures contained in the Emergency Response Plan;
v. Filing the ATS flight plan with the appropriate ATS unit;
vi. When applicable, signing the operational and ATS flight plans;
vii. Preparation and signing the Flight Release;
viii. Perform flight monitoring of the flights including notifying the appropriate ATS unit when the position of the aircraft cannot be determined by an aircraft tracking capability, and attempts to establish communication are unsuccessful
ix. Coordination of actions with Space Control/Reservations and Maintenance control (MCC) in respect of aircraft status, schedule changes, rerouting and positioning of aircraft for the entire network when deviations from planned operations occur.
x. Briefing of Crew on NOTAMS, Weather Flight Plan and any other factors that may be of concern to the flight Crew members.
xi. Calculation of RTOW/RLW and Payload for short notice flights.
xii. Operational control of flights within his jurisdiction.
xiii. Supervision of all Flight Operations Assistants (if engaged) in the Shift and the maintenance of a high standard of conduct and efficiency in the Operations Control. May act as Supervisor Operations Control in the Supervisor's absence from workplace.
xiv. Assume responsibility for Crew Accommodation, transports slips, Roster changes, and check-in, in the absence of crew scheduling staff.

## 2. POSITION: CREW SCHEDULING OFFICER II (2 POSTS)

### 2.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS

- Holder of a Bachelor Degree in any field.
- The candidate must have one of the following certificate; Air Transport Management, Air Ticketing, Air Cargo, Dangerous Goods, Ground Handling, or equivalent qualifications from any recognized Aviation institution.

### 2.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

Reporting to Supervisor Crew Scheduling, Crew Scheduling Officer shall have the following responsibilities;

**A: Planning Responsibilities**

i. To prepare monthly rosters for crew including training rosters taking into considerations the optimum utilization of crew in compliance to TCAA regulations and Company policy;
ii. To ensure a fair and equitable distribution of work among Flight Crew and Cabin Crew in terms of type of trips, number of flying hours and duty hours
iii. To ensure the day to day management and modification of the published rosters as per operational requirements;
iv. To provide solutions during flight disruption and ensure optimum utilization of crew;
v. Monitoring of Flight Crew and Cabin Crew published rosters, ensuring strict adherence to TCAA mandatory regulations;
vi. To maintains detailed records of flight times, rest times, holidays, sickness, and training, and 'deadhead' activities of crew members and enters / supervises the entry of such details into appropriate systems;
vii. Ensuring crew members are notified of any amendments to their published roster in a timely manner;
viii. To prepare monthly payments reports;
ix. To Prepare and monitor implementation annual leave plan

**B: Crewing Responsibilities**

i. To ensure the day to day management and modification of the published rosters as per operational requirements;
ii. To provide solutions during flight disruption and ensure optimum utilization of crew;
iii. Monitoring of Flight Crew and Cabin Crew published rosters, ensuring strict adherence to TCAA mandatory regulations;
iv. Ensuring that all flights are crewed in accordance with TCAA and company rules and regulations while maintaining company requirements;
v. Preparing daily duty sheet considering crew complaints, TCAA regulation and requirement of language speaker for all flights operated by Air Tanzania;
vi. Responds to absences, for reasons such as sickness, flight delays, etc. by rescheduling crew members at short notice. Call replacements, in coordination with the Operational Control;
vii. Ensuring members are notified of any amendments to their published roster in a timely manner.

## 3. POSITION: DRIVER II ( 37 POSTS )

### 3.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE:

- Must be a Holder of Form IV Certificate and a Class "C1 or E" Driving License who has attended Basic Driving Course offered by VETA or any recognized Institution
- Must have driving experience of at least one (1) year without causing accidents.
- Possession of Trade Test Grade II/Professional Level II in Motor Vehicle Maintenance/Mechanics is an added advantage.

### 3.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES:

i. Drive staff towards approved destinations in accordance with traffic regulations.
ii. Take vehicles due for routine maintenance / repair to the appointed service agents.
iii. Undertake minor mechanical repairs of motor vehicles.
iv. Maintain log books and records all movement as instructed.
v. Make routine inspection to the assigned vehicles to determine maintenance requirements
vi. Conduct pre-travel inspection for motor vehicle prior travelling and report mechanical damages / defects.
vii. Certify safety and cleanliness of the vehicle at all times.
viii. Verify that valid documents and permits are acquired prior commencement of any journey.
ix. Perform any other duty may be assigned by the supervisor.

## 4. POSITION: SALES AND MARKETING OFFICER II –TLO (2 POSTS)

### 4.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS:

- Bachelor Degree in any field.
- Must have one of the following certificates; Air Transport Management, Air Ticketing, or equivalent qualifications from any recognized Aviation institution.
- Possession certificate of IATA or UFTAA will be added advantage.

### 4.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

i. Supervise and ensure efficient and effective check in and boarding of passengers in compliance with carriers' policy/ procedures and customer expectations.
ii. Supervise baggage handling and prepare weekly baggage handling report. Liaise with the GHA to ensure lost baggage is communicated, traced and delivered to affected passengers.
iii. Ensure customers are well handled at all times and especially during flight irregularities and are provided with required assistance.
iv. Ensure conformity with all regulatory requirements, organization standards and local procedure as well as requirements of customer airlines.
v. Effective communication internally and externally to enable effective planning control and reporting
vi. Ensure a safe and secure working environment in compliance with relevant legislative/ industry requirements.
vii. Audit, review and report on service delivery to monitor compliance on SLA's availed to GHA.
viii. Administrative processes to ensure integrity and accuracy manual and computerized data processing.
ix. Strict control of excess baggage collection and remittance.
x. Record all flight movements as per company requirement.
xi. Any other duties as may be assigned by your supervisor.

## 5. POSITION: RAMP ASSISTANT II (12 POSTS)

### 5.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE:

- Must be a holder of a Certificate Secondary Education
- Must have a Certificate in aviation related course.
- Knowledge of the aviation industry and all airport ground support facilities will be an added advantage.

### 5.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES:

i. Gather, input and process all data and documentation required for the safe and secure turn-around, by manual, automated or computerized systems, including weather reporting and notams (if required), LDM, PSM, Special loads, cargo, mail, DGR, Steps, GPU, ASU, fuel, catering and crew change.
ii. Carry out pre-arrival inspections, aircraft and the aircraft footprint area hazard/FOD checks
iii. Lead the turn-around process, ensuring all relevant equipment, resources and services are in place, as required to complete a safe, secure and efficient, on time turn-around
iv. Ensure timely and effective communication with all relevant parties, both external and internal
v. Co-ordinate the safe, secure and efficient Customer disembarkation and boarding according to local procedures.
vi. Report any faults or irregularities with equipment, facilities, systems or processes to the appropriate management, airport authority and/or crew
vii. Provide timely and appropriate response and actions to disruption, emergency or delay situations in the operation
viii. Manage the offloading and loading procedures of the aircraft
ix. Perform accurate load reconciliation in line with approved guidelines and manuals
x. Communicate Aircraft movement messages and delay codes and assist with disruption management
xi. Assist in preparation of RC report and ensure the RC checklist is properly filled and filed.
xii. Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor

## 6. POSITION: SALES AND MARKETING ASSISTANT II (TLO)- (1 POST)

### 6.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS:

- Holder of Certificate in any field.
- Must have one of the following certificate; Air Transport Management, Air Ticketing, or equivalent qualifications from any recognized Aviation institution.
- Possession certificate of IATA or UFTAA will be added advantage.

### 6.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

i. Supervise and ensure efficient and effective check in and boarding of passengers in compliance with carriers' policy/ procedures and customer expectations.
ii. Supervise baggage handling and prepare weekly baggage handling report. Liaise with the GHA to ensure lost baggage is communicated, traced and delivered to affected passengers.
iii. Ensure customers are well handled at all times and especially during flight irregularities and are provided with required assistance.
iv. Ensure conformity with all regulatory requirements, organization standards and local procedure as well as requirements of customer airlines.
v. Effective communication internally and externally to enable effective planning control and reporting
vi. Ensure a safe and secure working environment in compliance with relevant legislative/ industry requirements.
vii. Audit, review and report on service delivery to monitor compliance on SLA's availed to GHA.
viii. Administrative processes to ensure integrity and accuracy manual and computerized data processing.
ix. Strict control of excess baggage collection and remittance.

## 7. TERMS AND CONDITIONS:

Ten (10) years contract for Tanzanians with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

## 8. GENERAL CONDITION FOR APPLICANTS:

i. All applications must be sent through ATCL Recruitment Portal by using the following address: https://recruitment.atcl.co.tz and NOT otherwise. This address can also be found at Air Tanzania website.
ii. Interested applicants must upload a dully signed letter for consideration of the application. The letter should be addressed to Managing Director & CEO, Air Tanzania Company Limited, P.O. Box 543, Dar es Salaam.
iii. An updated curriculum vitae (CV),
iv. Certified copies of all certificates (including secondary school birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania must have their certificates approved by relevant authorities (Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
v. Name and address of at least two reputable referees;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.
vii. Only shortlisted candidates will be informed on a date for interview
viii. Women are encouraged to apply.
ix. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.
x. Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

183464

# Kampeni msaada kisheria ya Samia yatua Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) leo inazinduliwa mkoani Kilimanjaro na itazifikia kata 10 katika kila halmashauri ndani ya siku tisa.

Katika kampeni hiyo, wananchi watapata elimu ya msaada wa kisheria na kutatuliwa migogoro inayohitaji usaidizi wa kisheria.

Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi, aliyasema hayo jana mjini hapa kwenye mafunzo ya wataalamu wa sheria watakaotoa huduma kwa wananchi kwenye kampeni hiyo.

Alisema kampeni hiyo itatoa huduma za msaada wa kisheria na kutatua migogoro inayohitaji usaidizi wa kisheria bure ili kujenga jamii yenye haki na usawa.

"Huu ni mkoa wa 17 kufikiwa na kampeni hii. Huduma hizi za msaada wa kisheria zinatolewa bure kabisa kwa kuwa serikali imegharamia," alisema.

Msambazi alitoa wito kwa wananchi kutumia fursa hiyo kupata elimu na msaada kwenye migogoro inayowakabili ya kisheria kwenye masuala ya ardhi, ndoa, mirathi na ukatili wa kijinsia.

Alisema watahakikisha maono ya Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya sheria yanatimia.

Kuhusu mafunzo kwa watoa huduma hiyo, mkurugenzi huyo alisema yametolewa kwa wataalamu ngazi ya halmashauri ili kuwa na uwezo wa kuendesha, kusimamia na kutathmini mpango wa kampeni hiyo kwa kuhakikisha wananchi wanapata msaada wa kisheria kwa urahisi, uwazi na ufanisi.

Mmoja wa wataalamu waliopata mafunzo hayo, Ofisa Ardhi Mteule wa Wilaya ya Same, Angelina Sampa, alisema wananchi wamekuwa hawana uelewa wa namna ya kusaidiwa kupata haki zao kisheria.

"Mafunzo ambayo tumeshiriki wilaya saba za Kilimanjaro zitatuwezesha sisi wataalamu na wale wanaohusika na masuala ya kisheria kuwahudumia wananchi. Tupo hapa maofisa maendeleo ya jamii, maofisa ardhi, wanasheria wa serikali, mawakili wa kujitegemea na wale wanaotoa msaada wa kisheria. Tunabadilishana uzoefu namna ya kutoa huduma bora na kuwafikia wananchi walipo," alisema.

Sampa alisema kuna wananchi wanaishi maeneo ya pembezoni wamekuwa wakihitaji msaada wa kisheria kwenye migogoro ya ndoa, mirathi, ukatili wa kijinsia na ardhi ili wapate ufumbuzi.

"Kampeni hii itawezesha wataalamu kufika ngazi ya vitongoji na vijiji kuwafikia wananchi na tutafanya mikutano ya hadhara, kutoa elimu na kuwasikiliza changamoto zao na namna watakavyopata suluhisho na matatizo yao," alisema.

Akizindua kampeni hiyo mkoani Kigoma hivi karibuni, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema wananchi 775,119 kwenye mikoa 11 wamefikiwa na kampeni hiyo na migogoro 3,162 ikiwamo ardhi, mirathi, ukatili wa kijinsia na ndoa imepokewa na kusikilizwa.

Ndumbaro alisema awamu hii itafanyika mikoa sita ya Kigoma, Geita, Tabora, Katavi, Mtwara na Kilimanjaro.

"Chimbuko la kampeni ni maelekezo ya Rais Samia ambaye aliona kiu ya wananchi ya kupata elimu ya kisheria na msaada wa kisheria. Pia ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (Chama Cha Mapinduzi) ya 2020-2025. CCM ilipita kwa wananchi na kuahidi kupitia ilani hii itapeleka elimu na msaada wa kisheria popote walipo," alisema Ndumbaro.

# Serikali yarahisisha utoaji hati za kusafiria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

Serikali imefunga mifumo ya kielektroniki katika ngazi za mikoa na wilaya ili kurahisisha upatikanaji wa hati za kusafiria na hati za dharura za safari, Bunge lilielezwa jana jijini hapa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kalambo (CCM), Josephat Kandege.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itaondoa usumbufu wa kupata vibali na gharama pale raia wa Tanzania wanapolazimika kushiriki shughuli za kijamii Zambia.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Sillo alisema hatua hiyo inalenga kuwaondolea usumbufu raia wa Tanzania pale wanapohitaji hati hizo kwa ajili ya kushiriki shughuli za kijamii katika nchi jirani.

"Kwa raia wanaoishi ndani ya eneo lisilozidi kilometa 10 kutoka mpaka wa nchi yetu na nchi jirani na wananchi wanapokuwa na shughuli za dharura kama vile misiba na magonjwa, hupatiwa ruhusa (vibali) maalum kuwawezesha kushiriki shughuli hizo," alisema.

Aidha, alisema kwa wale wanaokwenda nchi jirani kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, wanapaswa kufuata sheria na taratibu za nchi husika katika kulipia vibali vinavyoendana na shughuli wanazokwenda kufanya.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema kwa mtu wa kawaida ambaye anakwenda nchi jirani kushiriki shughuli za kijamii kutozwa Sh. 20,000 ambazo ni gharama kubwa na kuhoji kama serikali iko tayari kupunguza gharama hizo iwe Sh.5,000 au 2,000.

"Katika kufunga hii mifumo ya kielektroniki naomba kujua kama wilaya ya Kalambo ni miongoni mwao?" alihoji.



Naibu Waziri Sillo akijibu swali hilo, alisema tozo hiyo ya Sh.20,000 ipo kwa mujibu wa sheria na pale watakapoona kuna haja ya kupunguza serikali itafanyia kazi mapendekezo ya mbunge huku akisema wilaya hiyo imenufaika na mifumo hiyo.

**Kwa raia wanaoishi ndani ya eneo lisilozidi kilometa 10 kutoka mpaka wa nchi yetu na nchi jirani na wananchi wanapokuwa na shughuli za dharura kama vile misiba na magonjwa, hupatiwa ruhusa (vibali) maalum kuwawezesha kushiriki shughuli hizo.**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

SHAURI LA MADAI NA. 23668 YA 2024

TANG HANG DA COMPANY LTD.........................................MDAI

DHIDI YA

1. DODOMA CITY COUNCIL }
2. 2. THE ATTORNEY GENERAL }
3. ISAAC OKOTH KISSA }

KWA: ISAAC OKOTH KISSA

POPOTE PALE ULIPO,

YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA MADAI NA. 23668 YA 2024
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE. E. E. KAKOLAKI, JAJI** wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu na nusu (3:30) asubuhi siku ya Jumatano tarehe 12/2/2025 Hivyo; Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** Hutafika wewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughurikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 28 Novemba, 2024.

NAIBU MSAJILI
DODOMA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
YA WILAYA YA MOROGORO

KITUO CHA MJINI
MKOA WA MOROGORO

Usimamizi wa Mirathi Na...15/2025

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: GULIKO MADUKA wa MSAMVU "B" MOROGORO

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA SCHOLASTICA PASTORY

TANGAZO
(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 05 Mwezi 02 Mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 27 mwezi 01 mwaka 2025



KUPOTEA KWA CHETI



**MUSSA A. MBAROUK** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **P1377-0557** kilichotolewa **NATIONAL CORRESPONDENCE INSTITUTE** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/PWA/MKU/2479/2025.**



KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIREHEMA JEROME MREMA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya T**oyota Land Cruser Prado** yenye namba za usajili **T.618 CWC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MBE/MBE/1609/2025.**



IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 651 OF 2025

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE
GEORGE GERVAS MKINGA MPHERE

AND

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARTHA GEORGE MKINGA

GENERAL CITATION
(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 day of February, 2025.

Dated at KOROGWE this 10 day of January, 2025.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE



KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JASTINE JULIUS KATO Anatangaza** kupotelewa na kadi tatu za pikipiki na bajaji zenye namba za usajili **MC.846 AVQ** yenye Chassis **No.MD2A18AZXFWD51076** aina ya **BOXER, MC.670 BHZ** yenye Chassis No. **MBX0002CFSD876266 na MC.866 BLU** yenye Chassis No. **MBX0002CFRC864971** aina ya PIAGIO. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi; **PHQ/SHI/KAH/568/2025.**



KUPOTEA KWA PASSPORT



**ISSA CHARLES SHEBE** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye **NO.TAE434734** iliyotolewa tarehe 08 Novemba 2021 na kuisha muda wake tarehe 07 Novemba 2031. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/8724/2024.**



KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIREHEMA JEROME MREMA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya T**oyota Land Cruser Prado** yenye namba za usajili **T.618 CWC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MBE/MBE/1609/2025.**

## Hali tete Goma, Watanzania wakimbilia Rwanda

**Na Maulid Mmbaga**

VITA vimeendelea kushuhudiwa katika mji wa Goma Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) huku zaidi ya Watanzania 43 waliokwama na kuomba msaada kutokana na kuzingirwa na milio ya risasi wakifanikiwa kukimbilia Rwanda.

Machafuko katika mji huo yameendelea baada ya waasi wa M23 ambao inadaiwa kuwa wanashirikiana na wanajeshi wa Rwanda kuiteka Goma juzi na kuwalazimisha wanajeshi wa Kongo kujisalimisha, hali ambayo imesababisha wakazi kulikimbia eneo hilo.

Ilielezwa kuwa awali Watanzania hao walikuwa katika eneo la Jambo Safari karibu na Uwanja wa Ndege wa Goma walilazimika kuomba msaada wakihofia kuuliwa na waasi wa M23 baada ya kuvamia eneo hilo.

Kupitia video inayosambaa katika mitandao ya kijamii madereva hao walieleza kuwa hali haikuwa nzuri katika eneo walilokuwa wamejificha kwa takribani siku nne baada ya kukwama.

Mmoja wao aliyejitambulisha kama Aloyce Emmanuel ambaye ni dereva wa kampuni ya RMD alisema "tunaomba msaada sisi huku tulipo hali ni mbaya".

Wakati wakiendelea kuzungumza ilisikika milio ya risasi jambo linaloashiria wapo katika eneo ambalo si mbali na mapigano yanapoendelea.

Wakati huo huo, ilielezwa kuwa mpaka kati ya Rwanda na DRC karibu na mji wa Goma uliojaa majeshi umefungwa.

Wakati hayo yakijiri Rwanda ilikanusha kuhusika licha ya ripoti za kuaminika kutoka Umoja wa Mataifa (UN) zikionyesha kuwa taifa hilo linawaunga mkono M23.

"Mpaka umefungwa, hakuna anayekuja, wala anayeondoka, isipokuwa baadhi ya wafanyakazi wa UN na familia zao waliohamishwa asubuhi hii," alisema mfanyakazi wa misaada katika kivuko kikuu cha mpaka kati ya nchi hizo mbili.

Ilielezwa kuwa waasi pia wameufunga uwanja wa ndege wa Goma na kuchukua udhibiti wa kituo cha redio cha serikali.

Wakati huo huo, wakazi wa mjini Kinshasa wameandamana kupinga vita vinavyoendelea Goma dhidi ya waasi wa M23, ikielezwa kuwa waandamanaji hao wamechoka ubalozi wa Kenya na Ufaransa zilizoko katika mji huo.



Wakazi wa Mji wa Kinshasa DRC wakiandamana kupinga kinachoendelea Goma, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Miradi itakayoathirika Afrika, Marekani inapojiondoa WHO

**Na Maulid Mmbaga**

UAMUZI wa Rais wa Marekani, Donald Trump kuliondoa taifa hilo kuwa mwanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kunatazamiwa kuathiri programu zinazosimamiwa na shirika hilo katika bara la Afrika ikiwamo misaada ya kiafya na usalama barabarani.

Programu zingine ni Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya Umoja wa Mataifa ambayo yanalenga kupunguza idadi ya vifo na majeruhi kutokana na ajali za barabarani kote duniani.

Kuondoka kwa Marekani ambaye ni mfadhili mkuu wa shirika hilo, kunajiri wakati muongo wa pili wa utekelezaji, mpango wa Umoja wa Mataifa wa kupunguza vifo vya barabarani duniani kote na majeraha mabaya kwa asilimia 50 mwaka 2030, ukiwa umesalia miaka mitano tu.

WHO inakadiria kuwa majeraha na vifo vya barabarani barani Afrika vinagharimu angalau dola bilioni 12 (Sh. Trilioni 30) na bilioni 26 (Sh. Trilioni 65.7) kila mwaka. Na kwamba Afrika ndiyo mnufaika mkubwa wa shirika hilo katika masuala ya miradi ya usalama barabarani.

Mipango kama vile Mitaa Salama kwa Watumiaji Barabara barani Afrika, Usanifu wa Barabara Salama na Jumuishi, na Mpango wa Hatua Kumi wa Miundombinu ya Barabara Salama zote ni programu zinazofadhiliwa na Umoja wa Mataifa Afrika.

Sasa ni wakati Afrika kuelewa kwamba haiwezi kutegemea tu ufadhili kutoka WHO ili kufikia malengo yake ya maendeleo endelevu na malengo ya Muongo wa Pili wa Utekelezaji.

Licha ya Afrika, kuwa nchi za kipato cha chini hadi cha kati, na kutegemea sana UN kutunguliza usalama barabarani. Sasa inayo fursa ya kulipa suala la usalama barabarani kipaumbele kinachostahili.

WHO inasema kuna utafiti wa kutosha unaonyesha kwamba Afrika haifanyi vya kutosha kuwekeza katika utafiti wa usalama barabarani kama kanda.

Inasema gharama ya ajali za barabarani kwenye uchumi tayari ziko katika viwango vikubwa lakini haionekani ipasavyo katika uwekezaji wa utafiti wa usalama barabarani.

**NINI KIFANYIKE**

WHO inasema matumizi ya ziada na uwekezaji barani Afrika ni muhimu na kila nchi inapaswa kuweka malengo ya kutenga bajeti kuelekea utafiti na programu za usalama barabarani. Ikishauri kuwa kuongeza uwekezaji hatua kwa hatua ni bora kuliko kutokuwa na bajeti kabisa.

Inasema kuunda kihifadhi data na kumbukumbu ni muhimu kwa kusoma na kuchanganua mienendo ya usalama barabarani. Na kwamba zana hizo zina jukumu muhimu katika kufuatilia maendeleo na kutambua maeneo ya kuboresha.

"Kwa kuzingatia vikwazo vya bajeti vinavyokabili nchi nyingi, kushirikiana na sekta binafsi kunaweza kuimarisha juhudi za usalama barabarani. Sekta ya kibinafsi pia inaweza kusaidia kuziba mapungufu ya ujuzi yaliyopo.

"Pia kuhusisha vyuo vikuu na taasisi za utafiti katika utafiti wa usalama barabarani ni muhimu. Ushiriki wao unaweza kushughulikia masuala ya uwezo, katika suala la idadi ya wafanyakazi na ujuzi maalum," inapendekeza WHO.

Shirika hilo linaeleza kuwa usalama barabarani unahusisha sekta nyingi, na kwamba vyombo vya usalama barabarani vinapaswa kushirikiana na sekta kama vile afya, usafiri, fedha na vifaa ili kufanya utafiti bora na kuelewa masuala ya usalama barabarani.

Inasema baadhi ya masuala ya usalama barabarani yanaenea zaidi ya mipaka ya serikali, ikiimulika Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) kwamba inaweza kushiriki katika utafiti shirikishi ili kushughulikia matatizo hayo ya mipaka kwa ufanisi.

**MISAADA YA AFYA**

Hata hivyo, takriban ufadhili wote wa afya wa kimataifa kutoka Marekani umesitishwa na utawala wa Trump na hiyo inaonekana kujumuisha PEPFAR, ambao ni mpango wa ulioundwa na Rais George Bush mwaka 2003 kuzuia Virusi vya Ukimwi (VVU).

Takwimu za Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) zinaonyesha nchi 31 barani Afrika zinapata msaada kutoka Marekani kupitia USAID.

Miongoni mwa nchi hizo ni Tanzania iliyopata zaidi ya dola milioni 454 (Sh. Trilioni 1.1), Kenya zaidi ya dola milioni 702, Rwanda zaidi ya dola milioni 126, na Somalia zaidi ya dola bilioni moja.

Inaeleza kuwa Sudan Kusini ilipata zaidi ya dola milioni 800 na Sudan zaidi ya dola milioni 560.

Kwa mujibu wa USAID imesimamisha mikataba, ruzuku na makubaliano ya ushirika yanayosababisha kutokuwa na uhakika wa siku 60 hadi 90 kwa misaada tofauti barani Afrika.

"Katika mwaka wa fedha wa 2024, Marekani ilitoa karibu dola bilioni 6.6 kwa misaada kote Afrika," USAID inasema katika tovuti yake.

**MAMIA KURUDISHWA**

Wakati huo, Idara ya Uhamiaji ya Marekani imetangaza orodha ya nchi 208 dunaini ambazo wananchi wake 1,445,549 hawajakidhi vikezo vya kuishi nchini humo.

Katika taarifa hiyo iliyosambaa jana imeonesha kuna Watanzania 301 ambao hawana nyaraka zinazowaruhusu kuishi Marekani. Idara hiyo imezitaka nchi zenye raia hao kuwapokea watu wake ambao hawana sifa ya kuendelea kuishi Marekani.

Kwa ukanda wa Afrika Mashariki na SADC, nchi nyingine na idadi yake kwenye mabano ni Kenya ( 1,282); Rwanda (338); Somalia (4,090); Msumbiji (14); Botswana (12); Burundi (462); DRC (1,068); Eswatini (6); Malawi (5); Namibia (19) na Afrika Kusini (379). **CHANZO: MTANDAO**

# AZAM KUCHEZA MBILI ZA KIRAFIKI IKIIWINDA KMC

**Na Faustine Feliciane**

KLABU ya Azam imesema mechi za kirafiki wanazocheza ni mahususi kwa ajili ya kurejesha utimamu wa mwili kwa wachezaji wao kuelekea mchezo wao unaofuata wa Ligi Kuu mzunguko wa pili.

**Azam FC inatarajia kucheza mchezo wao wa pili wa Ligi Kuu mzunguko wa pili Februari 6, mwaka huu, dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa Azam Complex.**

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka za Kazi', alisema wameshacheza michezo miwili ya kirafiki na wanatarajia kucheza mingine miwili kabla ya mchezo wao na KMC.

"Tulicheza mchezo wa kirafiki na Mtibwa leo (jana) tunacheza na Uhamiaji ya Zanzibar na baadaye Januari 31 tutacheza na Mafunzo, lengo ni kurudisha utimamu kwa wachezaji watu kuelekea michezo ya Ligi Kuu," alisema Zaka.

Aidha, alisema anashukuru mpaka sasa hakuna majeruhi zaidi ya Lusajo Mwaikenda ambaye aliumia kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi akiwa na kikosi cha Kilimanjaro Stars.

"Majeruhi wengine wamerejea mazoezini, ila Lusajo bado yeye anatarajiwa kurejea uwanjani Machi, tunashukuru wachezaji wengine wote wanaendelea vizuri," alisema Zaka.

Alisema wanajiandaa kufanya vizuri kwenye michezo yao ya mzunguko wa pili na kocha wa timu hiyo, Rachid Taoussi, anaendelea kuwajenga wachezaji wake kwa mbinu mbalimbali.

"Tunaelekea kwenye mzunguko wa pili, mzunguko wa lala salama, tunataka kuhakikisha tunavuna pointi nyingi zaidi iwezekanavyo, tutarejea kwenye ligi tukiwa na nguvu na umara zaidi kwa sababu sisi hatukutoa mapumziko marefu baada ya ligi kusimama," alisema.

Azam inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 36 ikizidiwa na Yanga kwa pointi tatu ikiwa nafasi ya pili na vinara Simba wakiwazidi kwa pointi nne.

Hata hivyo, Azam imecheza mchezo mmoja zaidi ya Yanga na Simba zinazocheza michezo 15 kila moja.

## JKT Tanzania sasa yazipania Coastal, Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya JKT Tanzania imesema imejiwekea malengo ya kushinda michezo yake minne ya mwanzo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, inayotarajiwa kurejea tena, Februari Mosi, mwaka huu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Masau Bwire, amesema jana kuwa, baada ya mapumziko marefu, kikosi chao kimerejea kambini na wanachotaka sasa ni kuhakikisha wanapata ushindi katika michezo minne, dhidi ya Coastal Union, Yanga, Singida na KMC.

Ratiba ya timu hiyo inaonesha kuwa itaanza kucheza dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Februari 7, dhidi ya Yanga, Februari 10, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, kisha itaivaa Singida Black Stars, Februari 13 kwenye uwanja huo huo, kabla ya kwenda KMC Complex, kucheza dhidi ya wenyeji, KMC FC, Februari 18, mwaka huu.

Mechi ya mwisho ya Ligi Kuu ambayo JKT Tanzania ilicheza, ilikuwa ni Desemba 27, mwaka jana, ilipochapwa mabao 3-1, dhidi ya Azam FC, mechi ikipigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

"Malengo yetu ni kuchukua pointi 12 kwanza katika michezo hiyo minne, ambayo miwili tutacheza ugenini na miwili nyumbani. Labda watu wataona kama tunatania au haiwezekani kwa sababu ya kuangalia msimamo ulivyo, lakini ukweli ni kwamba tuna kikosi kizuri, tumekuwa na mechi nzuri sana mzunguko wa kwanza wakati mwingine bahati tu haiwi upande wetu, safari hii tumeongeza tena watu kwenye usajili wa dirisha dogo, hivyo tunajiamini tunaweza," alisema Masau.

Alisema anaamini kuwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu utakuwa mgumu kutokana na timu nyingi kuonekana kusajili wachezaji wengi wazuri, lakini wao pia watakuwa wazuri zaidi, chini ya Kocha Mkuu, Ahmad Ally.

JKT Tanzania ipo nafasi ya nane ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 19, kwa kucheza michezo 16, ikishinda minne, sare saba na kupoteza mitano, ikifunga mabao 10 na kuruhusu wavu wake kuguswa mara 12.

KIKAPU...



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya wenye ulemavu, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gaga aula tena KRFA

**Na Somoe Ng'itu**

ISAAC Munisi 'Gaga', amechaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Mkoa wa Kilimanjaro (KRFA), katika uchaguzi wa chama hicho uliofanyika juzi mkoani humo.

Gaga amepita pila kupingwa baada ya kuthibitishwa kwa kura zote za ndio na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa KRFA.

Nafasi ya Makamu Mwenyekiti ilikwenda kwa Dk. Daudi Mavura na Katibu Mkuu mpya aliyeteuliwa ni Deogratius Lawrence.

Walioshinda katika nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Utendaji ni pamoja na Thabit Abdallah, Hamad Hassan, Jaffari Kyango na Agness Kessy.

"Ninawashukuru sana wajumbe wa mkutano mkuu kwa kuniamini tena kuiongoza KRFA, nitahakikisha kwa pamoja tunashirikiana ili kufikia malengo ya kurejesha heshima ya mkoa wa Kilimanjaro.

"Tunajua kiu ya Wana-Kilimanjaro ni kuona tunapata timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara. Lakini pia tumekuwa na mikakati imara ya kukuza soka la wanawake. Tunaahidi tutaanza mwaka huu kuwa na Ligi ya Mkoa ya Wanawake yenye idadi kubwa ya timu, lakini pia wachezaji wakipata idadi zaidi ya mechi," alisema Gaga.

Kwa mujibu wa Katiba ya KRFA, viongozi hao waliochaguliwa watakaa madarakani kwa muda wa miaka minne.

## Nchi 8 kuchuana vishada Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya washiriki 39 kutoka nchi nane wanatarajia kushiriki mashindano ya kimataifa ya mchezo wa resi wa kurusha vishada baharini yatakayofanyika visiwani hapa.

Mashindano hayo yamepangwa kufanyika Februari Mosi, mwaka huu, kwenye ufukwe wa Kiwengwa uliopo Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BMTZ ), Said Marine, alisema mashindano hayo yamepewa jina la (Zanzibar Cup Kaskazi 2025) ikiwa huu ni mwaka wa tatu yanafanyika tangu yalipoanza kwa mara ya kwanza mwaka 2023.

Marine alisema mashindano hayo yameandaliwa na BMTZ kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar ikiwa na lengo la kuendelea kuwavutia watalii wanaofika Zanzibar.

"Kwa mwaka huu tumepata haya mataifa nane, kati ya washiriki 39, wanawake ni watatu, ingawa idadi yao ni ndogo, lakini angalau tumepata washiriki hawa, matumaini yangu mwaka ujao idadi ya wanawake itaongezeka," alisema Marine.

## ZISIKUPITE

### NKUNKU ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United huenda ikamnunua mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27, kwa mkopo ikiwa Marcus Rashford mwenye miaka 27 ataondoka katika klabu hiyo. ***(The Athletic)***

### MCATEE KWA MKOPO

KLABU ya Bayer Leverkusen imefanya mawasiliano na Manchester City kuhusu uhamisho wa mkopo wa kiungo wa kati wa England, James McAtee, 22. ***(Daily Mail)***

### BUENDIA KWA MKOPO

KIUNGO wa kati wa Argentina, Emiliano Buendia mwenye umri wa miaka 28, yuko mbioni kujiunga na Leverkusen kutoka Aston Villa kwa mkopo. ***(Florian Plettenberg)***

### DURAN ATAKIWA AL-NASSR

MSHAMBULIAJI wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 21, analengwa na Klabu ya Saudi Arabia ya Al-Nassr kwa euro 100 wakati wanatafuta mshirika mpya wa Cristiano Ronaldo. ***(Football Transfers)***

### DANSO AWINDWA WOLVES

KLABU ya Wolves ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa Lens na Austria mwenye thamani ya pauni milioni 16, Kevin Danso, 26. ***(Telegraph)***

### ADEYEMI AGOMBEWA

LIVERPOOL na Chelsea ziko tayari kuchuana na Napoli kwa ajili ya kumnunua fowadi wa Borussia Dortmund na Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 23, lakini wanaweza kusubiri hadi msimu wa majira ya joto kufanya uhamisho. ***(Corriere Dello Sport)***

### HUIJSEN AVUTIA VIGOGO

REAL Madrid, Bayern Munich na Juventus zinavutiwa na beki wa Bournemouth, Dean Huijsen, 21. ***(Fichajes)***

### SESKO ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inafikiria kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 21 na mshambuliaji wa Bayern Munich na Ufaransa, Mathys Tel, 19. ***(TeamTalk)***

### ZABARNYI AWANIWA

KLABU ya Newcastle United inavutiwa na mlinzi wa Kimataifa wa Ukraine, Illia Zabarnyi mwenye umri wa miaka 22, lakini wanajua kuwa dili halitawezekana hadi msimu wa majira ya joto. ***(i Paper)***


### DISASI, VILLA WAKUBALIANA

ASTON Villa imefikia makubaliano binafsi na beki wa Chelsea na Ufaransa, Axel Disasi, 26. ***(Fabrizio Romano)***

### FELIX NAYE AVUTIWA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 25, pia anavutiwa na Aston Villa. ***(Sportsport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR AONDOKA RASMI AL HILAL, KUTUA SANTOS

**JEDDAH,** Saudi Arabia

● ● ● Akubali kupoteza dola milioni 30, huku akitarajiwa kutangazwa klabu yake hiyo mpya kati ya...

AL Hilal imetangaza kuwa imefikia makubaliano na Neymar kusitisha mkataba wake na kufungua mlango wa kurejea Santos kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil.

**Klabu hiyo ya Ligi Kuu Saudi Arabia ilisema jana kwenye mitandao ya kijamii kwamba pande hizo mbili zimekubaliana kuachana na kumtakia Neymar mafanikio katika maisha yake mengine ya baadaye.**

Mustakabali huo unazidi kuonekana kama utakuwa katika nchi yake ya asili ya Brazil, vyanzo vya ESPN vilisema Jumapili kwamba Neymar atasaini mkataba wa miezi sita na chaguo la nyongeza ya mwaka, timu ambayo ndiko alikoanza kucheza akiwa kijana mdogo.

Kwa mujibu wa ESPN Brazil, Neymar anatazamiwa kusaini mkataba na Santos siku zijazo, na klabu hiyo inapanga kumtambulisha kwa mashabiki kesho Alhamisi au Ijumaa.

Ili kurahisisha kurejea kwake, Neymar amekubali kutoa sehemu kubwa ya mshahara wake kutokana na mkataba wake na Al Hilal, ambao ulikuwa ukamilika msimu ujao wa majira ya joto.

Vyanzo vya habari vilisema atapoteza kati ya dola milioni 25 na milioni 30 kutoka dola milioni 65 zilizobaki kwenye mkataba wake.

Neymar mwenye umri wa miaka 32, alivumilia kipindi kigumu akiwa na Al Hilal baada ya kujiunga na klabu hiyo ya Saudi Arabia kutoka Paris Saint-Germain msimu wa majira joto wa 2023 kwa ada ya dola milioni 97.6.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona alipata majeraha ya goti lake la kushoto akiwa kwenye majukumu ya kimataifa muda mfupi baada ya kusajiliwa na Al Hilal.

Alirejea uwanjani Oktoba mwaka jana, lakini jeraha la msuli lilimzuia kutoa mchango zaidi, na kocha Jorge Jesus, alisema mapema Januari kwamba Neymar alikuwa huru kutafuta nafasi nyingine.

Alicheza mechi saba tu za ligi akiwa na bao moja pekee katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa ya Asia dhidi ya Nassaji Mazandaran mnamo Oktoba 3, 2023.

## HABARI MICHEZO

CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

# NAFASI ZA KAZI

Chama cha Walimu Tanzania ni Chama cha Wafanyakazi kutoka kada ya Walimu ambacho shughuli zake zipo Tanzania Bara tu. Chama kimesajiliwa kwa Namba 004 chini ya Sheria na Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004 na kinaajiri Wafanyakazi kwa ajira ya kudumu ambao wapo katika kila mkoa. Ili kuboresha huduma bora kwa wanachama, zoezi la kuajiri kadri ya uhitaji halikwepeki. Hivyo Chama cha Walimu Tanzania kinahitaji kupata rasilimali watu wenye taaluma kadri ya nafasi zilizopo katika ofisi za Chama Makao Makuu yaliyopo Jijini Dodoma.

### 1. AFISA HABARI NA MAHUSIANO – NAFASI 1

**Majukumu ya kazi**
- Kukusanya na kuandika Habari
- Kupiga picha za matukio mbalimbali ya Taasisi
- Kuandaa picha za maonesho
- Kuandaa majarida na mabango
- Kukusanya takwimu mbalimbali
- Kuandaa majarida na vipeperushi
- Kuhifadhi picha, kuhudumia maktaba na marejeo
- Kufuatilia na kujibu hoja mbalimbali zinazotelewa dhidi ya chama
- Kuandaa mahojiano baina ya viongozi wa Chama na vyombo vya Habari
- Kuhakikisha kunakuwa na Habari sahihi na kwa wakati
- Kutoa taarifa kwa vyombo vya Habari juu ya matukio mbalimbali ya CWT kwa kibali cha Mkuu wa kazi
- Kujibu hoja mbalimbali za wanachama na wadau wanaouliza masuala yahusuyo Chama cha Walimu kupitia simu na barua pepe za Chama
- Kufanya kazi nyingine kama atakavyoagizwa na msimamizi wake wa kazi.

**Sifa za mwombaji**
- Awe na Shahada ya Kwanza au Stashahada ya juu ya Mahusiano ya Umma na Uandishi wa Habari au sifa inayolingana nayo kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali
- Awe na uwezo wa kuandika na kuzungumza lugha ya Kiswahili na Kiingereza
- Awe mfuatiliaji mzuri na mwelewa wa taarifa na matukio mbalimbali juu ya masuala ya Walimu na Vyama vya Wafanyakazi
- Awe na uwezo wa kutumia computa

### 2. MHASIBU – NAFASI 2

**Majukumu ya Kazi**
- Kufanya shughuli zote za fedha
- Kufanya malinganisho ya mapato na matumizi ya kila siku
- Kuandaa hesabu za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima
- Kufanya malipo yote yaliyoidhinishwa
- Kujibu hoja za ukaguzi
- Kuandaa hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha
- Kuandaa taarifa za ukaguzi wa fedha za mwaka
- Kusimamia na kuthibitisha malipo
- Kufanya kazi nyingine kama atakavyoagizwa na msimamizi wake wa kazi

**Sifa za Mwombaji**
- Awe na Stashahada ya juu au Shahada ya Uhasibu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta
- Mwenye uwezo wa kutumia mifumo ya kompyuta ya kiuhasibu
- Kuajiriwa mwenye Shahada ya Uzamili ya Uhasibu/Biashara yenye mwelekeo wa Uhasibu kutoka Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

### 3. MKAGUZI WA NDANI – NAFASI 1

**Sifa za Mwombaji**
- Awe na Shahada ya Uhasibu/Stashahada ya Juu ya Uhasibu/Ukaguzi wa Hesabu wenye Cheti cha Taaluma ya Uhasibu CPA (T) au sifa nyingine zinazotambulika na NBAA.
- Awe na uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa Ufasaha.
- Awe na uzoefu wa kutumia kompyuta.
- Awe na uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu

**Majukumu ya kazi**
- Kuandaa program ya ukaguzi wa ndani
- Kufanya chambuzi katika hatua za awali za ukaguzi
- Kufanya tathmini za udhibiti wa mifumo ya ndani katika hatua za awali (Internal Controls), udhibiti wa vihatarishi (Risk Management) na usimamizi wa mifumo ya uendeshaji (Corporate Governance).
- Kufanya ukaguzi wa kawaida, maalum, kiufundi na uchunguzi (Normal Audit, Special Audit, Technical Audit and Invetigations).
- Kuandaa mpango wa ukaguzi wa ndani wa kawaida au Maalum
- Kufanya uhakiki wa hoja za ukaguzi zilizopokelewa
- Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ndani
- Kutoa ushauri wa kuimarisha utendaji wa Taasisi.

### 4. KATIBU MUHTASI – NAFASI 17

**Majukumu ya kazi**
- Kupiga chapa nyaraka mbalimbali za Chama
- Kutunza kumbukumbu mbalimbali kama atakavyoelekezwa na mkuu wake wa kazi
- Kupokea wageni na kuwaelekeza mahali wanapoweza kusaidiwa.
- Kupokea mawasiliano mbalimbali ya ofisi na kumpatia msimamizi wa kazi.
- Kufanya usafi ofisi za chama
- Kutunza siri zote za ofisi
- Kufanya kazi nyingine atazopangiwa na msimamizi wa kazi

**Sifa za Mwombaji**
- Awe na Cheti (NTA level 5) au Stashahada (NTA level 6) ya Uhazili inayotambuliwa na NACTE.
- Awe amehitimu kidato cha nne au zaidi.
- Awe na uzoefu wa kutumia kompyuta na matumizi ya Intaneti.
- Awe na uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha.

### 5. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
2. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa
3. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V)
4. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Viambatisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea
5. Cheti cha Kuhitimu Kidato cha IV na VI
6. Vyeti vya kitaaluma
7. Picha moja "Passport size) ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma
8. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA)
9. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
10. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
11. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza
12. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19 Februari, 2025 saa 10:00 Jioni kupitia anuani ifuatayo:-

**Katibu Mkuu,**
**Chama cha Walimu Tanzania,**
**Mtaa wa Jamhuri**
**S.L.P 3077,**
**DODOMA.**
**Barua pepe: info@ttu.or.tz**

**Imetolewa na:**

KATIBU MKUU
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
MAKAO MAKUU - DODOMA

Mwl. Joseph M. Misalaba
KAIMU KATIBU MKUU - CWT

# VAN DIJK: BADO SIJUI HATIMA YANGU LIVER




**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Virgil van Dijk, amekiri kwamba bado kuna sintofahamu juu ya mustakabali wake katika klabu hiyo, huku mkataba wake ukiwa unakaribia kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Van Dijk amekuwa mchezaji wa Liverpool kwa miaka saba, na kufikisha mechi yake ya 300 kwa klabu hiyo katika ushindi wa Jumamosi wa Ligi Kuu England dhidi ya Ipswich Town.

Lakini baada ya kuingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake uliopo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, tayari anastahili kufanya mazungumzo na klabu nyingine na amesisitiza kuwa "hajui" ni mechi ngapi zaidi atakazoongeza kwenye idadi ya mechi zake za sasa akiwa Liverpool.

"Je, ni mechi ngapi zilizosalia msimu huu? Natumaini hizo zimehakikishwa na sijui siku zijazo zitaleta nini," alisema Van Dijk.

Mholanzi huyo ana asilimia kubwa ya ushindi kuliko mchezaji yeyote wa Liverpool ambaye amecheza mara 300 au zaidi kwenye klabu hiyo na anajivunia mafanikio yake.

"Hiyo inaonesha nilifanya vema hadi sasa. Inategemea kila mtu aliyehusika - wachezaji, wasimamizi, mashabiki. Ni takwimu nzuri kuwa nazo. Tutaendelea. Ushindi mzuri kwa hiyo sasa tunazingatia inayofuata," alisema.

# Fuente kuinoa Hispania hadi 2028

**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Hispania, Luis de la Fuente, atabakia kuinoa timu hiyo ya taifa hadi mwaka 2028, Shirikisho la Soka (RFEF), limetangaza.

Mkataba wa awali wa De la Fuente ulikuwa unaisha baada ya Kombe la Dunia la 2026.

Mkataba huo mpya na ulioboreshwa utamwezesha kocha huyo mwenye umri wa miaka 63 kuiongoza timu kwenye michuano ya Ulaya 2028.

"Jambo hili ni bora," alisema De la Fuente.

"Ninahisi niko nyumbani hapa. Nipo ninapotaka kuwa na sikuwahi kufikiria chaguo lingine. Tuna nia ya kuendelea kushinda. Hiyo ndiyo mawazo tunayopaswa kuwa nayo. "Hii inapaswa kuwa motisha yetu. Ni kuboresha mara kwa mara. Tuna msingi wa kuvutia, mawazo yasiyotosheka katika kiwango cha michezo.

"Nadhani tutapigania mambo muhimu sana. Tutajitolea katika mashindano yote ili kutwaa mataji mengi zaidi. Natumaini kuna ushindi zaidi, kwa umoja tuna nguvu zaidi. Tumejaribu kueleza kuwa sisi ni familia, kwamba sisi sote."



Kocha huyo wa zamani wa Alaves alichukua nafasi ya Luis Enrique kama kocha mnamo Desemba 2022 kutokana na Hispania kutolewa katika hatua ya 16-bora kwenye Kombe la Dunia.

Hapo awali alifundisha timu ya Hispania chini ya umri wa miaka miaka 21, na pia aliongoza timu ya Olimpiki kutwaa medali ya fedha kwenye Michezo ya Olimpiki ya 2022 huko Tokyo.

## HABARI MICHEZO

## Stars: Hatuihofii Nigeria

INATOKA UKURASA 24

Michezo itachezwa katika miji sita: Agadir, Casablanca, Fez, Marrakesh, Rabat na Tangier.

Washindi wawili wa juu katika kila kundi pamoja na washindi wanne bora waliomaliza katika nafasi ya tatu wataingia katika hatua ya 16 bora.

**Droo kamili:**
**Kundi A:** Morocco, Mali, Zambia, Comoro
**Kundi B:** Misri, Afrika Kusini, Angola, Zimbabwe
**Kundi C:** Nigeria, Tunisia, Uganda, Tanzania
**Kundi D:** Senegal, DR Congo, Benin, Botswana
**Kundi E:** Algeria, Burkina Faso, Equatorial Guinea, Sudan

## Fadlu awataka mabeki Simba

INATOKA UKURASA 24

kwa maana hiyo hapo tupo vizuri, baadaye nikaanza kazi ya kufanya kwa mabeki wangu wasiwe wanafanya makosa binafsi ambayo yanasababisha turuhusu mabao mepesi.

"Tumeona kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya CS Constantine, pia Kombe la FA dhidi ya Kilimanjaro Wonders, hatukuruhusu bao, liwe la binafsi au la mfumo," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema katika michezo mingi ya ugenini ya Ligi Kuu ambayo Simba ilicheza nje ya Dar es Salaam, iliruhusu mabao mawili tu dhidi ya Kagera Sugar, uliochezwa Desemba 21, mwaka jana, ambao walishinda 5-2.

"Tumecheza mechi za nje, huko mara nyingi tumepata ushindi wa mabao machache na hatukuwa tunaruhusu sana mabao, hii inaonesha staili yetu pia inategemea na viwanja tunavyocheza, kuna vingine haviruhusu kucheza sana nyuma," alisema kocha huyo.

Alisema kama mabeki wake watacheza kama walivyofanya katika michezo hiyo miwili, wana uhakika wa ushindi kwani hawatoruhusu wavu wao kuguswa na pia wana uhakika wa kupata bao moja au zaidi kwenye mchezo huo.

Wakati huo huo wachezaji wote wa Simba waliokuwa wemepewa mapumziko baada ya majukumu ya mechi za kimataifa wamerejea na jana wamefanya mazoezi ya pamoja kujiandaa na mchezo huo dhidi ya Tabora United.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema baada ya mchezo wao wa mwisho wa Kombe la Shirikisho hatua ya makundi dhidi ya CS Costanine, Simba iliwapa mapumziko wachezaji wote waliohusika katika mchezo huo ambapo mapumziko yao yameisha juzi na jana wote walihudhuria mazoezi ya timu hiyo.

# RAMOVIC ATAKA KUZOA MAKOMBE YOTE BONGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI makocha wa timu zingine wakifikiria kutwaa ubingwa msimu huu, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, ameibuka na kusema anataka kuweka rekodi ya kuzoa makombe yote ya hapa nchini kwa mara ya kwanza kwenye historia yake ya soka.

**Kocha huyo ameyasema hayo siku chache kabla ya kuelekea kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa, Jumamosi kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, dhidi ya Kagera Sugar.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ramovic, alisema baada ya kuondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kikosi chake kitakuwa na muda wa kujiandaa kwa ajili ya michezo ya ndani ambayo hataki kuacha kombe hata moja.

Alisema Yanga ndiyo inayoshikilia makombe yote ya ndani, hivyo atahakikisha yanabaki, huku yeye mwenyewe akitaka kuweka rekodi ya kuyachukua kwa mara ya kwanza akiifundisha timu hiyo kongwe nchini.

"Tunataka kushinda kila kitu, tunataka kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA, tumeshatolewa kwenye michuano ya kimataifa, nadhani sasa tuna muda mzuri wa kujiandaa.

Inabidi sasa nguvu zetu zielekezwe huku, huu ndiyo mkakati ambao sasa tunao, na ili ifanikiwe tunatakiwa kushinda kila mchezo ulio mbele yetu, uwe wa Ligi Kuu au Kombe la FA, miguu ya wachezaji wetu inatakiwa kuwa na nguvu, ikimbie kilometa nyingi," alisema.

Alisema yeye kama kocha kazi yake itakuwa moja tu kuwaelekeza wachezaji wake kwenye uwanja wa mazoezi nini cha kufanya watakapokuwa uwanjani, kwani na yeye anataka kuwapa rekodi yake.

"Kama kocha ni lazima unapokwenda sehemu na wewe uache alama," alisema kocha huyo ambaye alichukua nafasi ya Miguel Gamondi.

Ramovic, ameiongoza Yanga kucheza michezo mitano ya Ligi Kuu, akishinda yote, ambapo Jumamosi wiki hii ataiongoza kwenye mechi ya sita.

Alianza kuiongoza kwenye mchezo dhidi ya Namungo FC, uliopigwa Novemba 30, mwaka jana, Uwanja wa Ruangwa, Lindi, ikishinda mabao 2-0, Desemba 19, mwaka jana, kwenye Uwanja wa KMC Complex ikaizamisha Mashujaa FC 3-2, kisha ikaikanda Prisons 4-0, Desemba 22, mwaka jana, uwanja huo huo, kabla ya kwenda jijini Dodoma na kutoa kipigo kama hicho dhidi ya Dodoma Jiji na kumalizia kwa kutoa dozi ya mabao 5-0 dhidi ya Fountain Gate, Desemba 29, mwaka jana.

Utakuwa ni mchezo wa mzunguko wa pili, ambapo wa kwanza ulichezwa Agosti 29, mwaka jana, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, Yanga ikipata ushindi wa mabao 2-0 yaliyofungwa na Maxi Nzengeli na Clement Mzize.




Kocha wa Yanga, Sead Ramovic

## *Namungo yaahidi kurejea kwa kishindo lala salama*

**Na Somoe Ng'itu**

KUELEKEA mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuendelea tena kuanzia Februari Mosi, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Juma Mgunda amesema "tumeimarika".

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema mapumziko yaliyopatikana yamemsaidia kufanyia kazi mapungufu mbalimbali aliyoyabaini katika kikosi chake.

Mgunda alisema ametoa programu maalumu kwa kila idara kwa sababu anahitaji kupata matokeo mazuri katika michezo yote ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

"Tumefanyia kazi mambo mbalimbali, kila unapofanya mazoezi, unapata nafasi ya kuelekeza mbinu mpya, tuseme mapumziko ya ligi yamekuwa na tafsiri chanya upande wetu, yametusaidia kujiimarisha, sasa tuko tayari kuendelea na mapambano," alisema Mgunda.

Nahodha wa timu hiyo, Erasto Nyoni, aliliambia gazeti hili wamejipanga kurejesha furaha kwa mashabiki wao ambao hawakushuhudia mambo mazuri katika kikosi chao kwenye mechi za awali za msimu.

Beki huyo wa zamani wa Azam FC na Simba, alisema wachezaji wote wamejiandaa kukutana na ushindani katika hatua hiyo ya pili kwa sababu kila upande unahitaji kutimiza malengo yake.

"Hatukuwa na mwendelezo mzuri, tumepitia wakati mgumu, lakini sasa tunaahidi kurejea kwa furaha, tunajua haitakuwa rahisi, lakini tuko tayari kuipambania timu yetu na hatimaye kufikia malengo," beki huyo mkongwe alisema.


Aliongeza hawatabweteka na mechi yoyote na wanafahamu hakutakuwa na mchezo mwepesi.

"Kila timu itaingia uwanjani ikiwa imejipanga kusaka ushindi au sare na si kupoteza, hapa ndio panapoongeza ugumu, hakuna timu itakayoingia uwanjani na matokeo yake, hivyo ili kupata ushindi ni lazima uwe bora," Nyoni aliongeza.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Namungo FC yenye pointi 17 iko nafasi ya 12, imeshinda michezo mitano, sare mbili na imepoteza mechi tano msimu huu.

Simba yenye pointi 40 ndio vinara wa ligi hiyo yenye timu 16 huku mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 39 inafuatia katika msimamo huo, wakati KenGold ya jijini Mbeya ikiburuza mkia na pointi zake sita kibindoni.

Michezo
Jumatano Januari 29, 2025
Nipashe



Neymar aondoka rasmi Al Hilal UKURASA 21

WATAKABIKA TU...




Washambuliaji hatari wa Nigeria, Ademola Lookman na Victor Osimhen, ambao kama watakuwa fiti na kuitwa timu ya taifa hilo kwenye fainali za AFCON 2025 nchini Morocco, mabeki wa Taifa Stars watakuwa na kibarua kigumu kukabiliana nao. Lookman anaichezea Atalanta ya Ligi Kuu Italia wakati Osimhen akikipiga kwa mkopo Galatasaray ya Uturuki akitokea Napoli ya Italia. **PICHA: MTANDAO**

# Stars: Hatuihofii Nigeria, Tunisia AFCON Morocco

**Dennis Fussi na Adam**

**Fungamwango**

●●● Ni wakati Wanaigeria hao wakiwa na nyota kama Ademola Lookman na Victor Osimhen, Watanzania watolewa...

BAADA ya droo ya makundi ya fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, zitakazofanyika mwakani nchini Morocco kutoka juzi, huku Tanzania ikiangukia Kundi C pamoja na Nigeria, Tunisia na Uganda, benchi la ufundi la Taifa Stars limesema halihofii hata kidogo timu walizopangwa nazo, badala yake watapambana kuhakikisha wanasonga mbele na kufuzu hatua zinazofuata.

**Mmoja wa makocha wasaidizi wa Taifa Stars, Jamhuri Kihwelo 'Julio', akizungumza kutoka nchini Morocco ambako droo hiyo ilipangwa kwa timu zote 24 zilizotinga fainali hizo, alisema kinachotakiwa ni kujipanga na kuhakikisha wanachagua timu imara ya kuweza kupambana, licha ya kuwapo kwa timu kama Nigeria na Tunisia.**

Licha ya Nigeria, iliyotinga fainali mwaka jana ikiwa na washambuliaji nyota kama Ademola Lookman na Victor Osimhen, Julio alisema anashangaa kuona baadhi ya mashabiki wa soka nchini kwenye mitandao ya kijamii wameanza kuwakatisha tamaa kwa kudai kundi hilo ni gumu badala ya kuwatia moyo.

"Sijaona sehemu yoyote kama kuna kundi jepesi, makundi yote ni magumu, kinachotakiwa Watanzania ni kutiana moyo, kujiandaa kwa ajili ya kupambana ili kufanya vizuri, lakini nimeanza kuona kwenye mitandao watu wakisema maneno mengi kuwa kundi ni gumu, hatuwezi, tutaenda kushiriki tu, lakini tulipofuzu fainali hizi hakuna mtu yoyote aliyetusifia," alisema kocha huyo.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni Watanzania kuungana na kila mmoja achukue nafasi yake ili kujiandaa na fainali hizo badala ya kutishana au kukatishana tamaa.

"Nadhani kwa hili Watanzania wote inabidi mtuunge mkono sisi watu wa benchi la ufundi na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), kwa ujumla ili tuwapambanie kwa hili ambalo limetokea, matokeo yake wameona kama vile tumeshatolewa, ikumbukwe tumefuzu kwa kuifunga timu ngumu ya Guinea, sisi kama makocha chini ya Hamed Suleiman 'Morocco', tuna imani kuwa tunapambana kwa ajili ya kufanya vizuri.

"Hatuhofii timu yoyote, ukiwa katika michuano kama hii, timu kama hizo ni lazima ucheze nazo, huwezi kupewa timu mchekea zote, na sisi pia Tanzania tumeshakuwa timu kubwa sasa, tutapambana kuhakikisha tunafuzu," alisema Julio.

Katika droo hiyo, Ivory Coast itaanza kutetea taji lake la Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya Msumbiji, huku wenyeji Morocco na waliofuzu nusu fainali Kombe la Dunia 2022, watafungua michuano hiyo dhidi ya Visiwa vya Comoro mjini Rabat Desemba 21, mwaka huu.

Michuano hiyo itaanza Desemba 21 hadi Januari 18 nchini Morocco kabla ya nchi hiyo kuandaa Kombe la Dunia la 2030 pamoja na Hispania na Ureno - timu walizoziondoa kwenye Kombe la Dunia la 2022 na kuwa taifa la kwanza la Afrika kuwahi kufika nusu fainali kabla ya kufungwa na Ufaransa.

Katika Kombe la Afrika lililopita, mwaka mmoja uliopita, Morocco ilitolewa kwa mshangao katika hatua ya 16-bora na Afrika Kusini.

Ivory Coast ilishinda Kombe hilo la Afrika kama taifa mwenyeji na wataanza kutetea ubingwa wao katika kundi moja na Cameroon, Gabon na Msumbiji.

Misri yenye nyota Mohamed Salah ambaye analitafuta taji la kwanza la Kombe la Afrika, atakuwa na umri wa miaka 33, wakati michezo inaanza Desemba, ikipangwa kundi moja na Afrika Kusini, Angola na Zimbabwe.

Senegal, bingwa wa mwaka 2021 atamenyana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Benin na Botswana wakati Algeria ipo Kundi E pamoja na Burkina Faso, Equatorial Guinea na Sudan.

INAENDELEA UKURASA 23

## Fadlu awataka mabeki Simba kuamua mechi Tabora United

**Faustine Feliciane na Adam**

**Fungamwango**

WAKATI wachezaji wote wa Simba waliokuwa wemepewa mapumziko baada ya majukumu ya mechi za kimataifa wakirejea jana na kufanya mazoezi ya pamoja kujiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu mzunguko wa pili dhidi ya Tabora United, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema safu yake ya ulinzi ndiyo itakayoubeba zaidi mchezo huo Jumapili wiki hii.

Timu hizo zinakutana Jumapili katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora, Simba ikiwa na kumbukumbu ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza uliopigwa Agosti 18, mwaka jana, Dimba la KMC Complex, Dar es Salaam, yaliyofungwa na Che Fondoh Malone, Valentino Mashaka na Awesu Awesu.

Akizungumza kuelekea kwenye mchezo huo, Fadlu alisema kwa sasa safu yake ya ulinzi imezidi kuimarika, ikiwa haina rekodi ya kuruhusu sana mabao kwenye viwanja vya ugenini, kitu kinachomfanya kuwa na imani ya kufanya vizuri katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema anatarajia utakuwa mgumu kama ilivyokuwa michezo mingine ya ligi huko nyuma, lakini anakiona kikosi chake kikiimarisha siku hadi siku, hasa kila kinapocheza michezo ya kimataifa, huku sehemu ya ulinzi ikiwa imara zaidi.

Fadlu alifafanua kuwa hapo nyuma kidogo kulikuwa na matatizo ya kuruhusu bao au mabao hata kama timu ikishinda, lakini kwa sasa hali hiyo imetengemaa, jambo ambalo ni zuri kwenye mchezo wa soka.

"Tumekuwa tukiruhusu mabao ambayo ukiyaangalia ni ya makosa binafsi ya mchezo mmoja mmoja, ina maana hatukuwa tunaruhusu mabao ya kimfumo

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >